# LUGHA KATIKA IDARA YA UHAMIAJI NCHINI KENYA: MFANO WA IDARA YA UHAMIAJI MOMBASA

NA

TIMOTHY MALASI OTUCHI.

C50/68469/13

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA SEHEMU YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

OKTOBA 2017

A1701593A
University of Nairobi Library Thesis
2016

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijatolewa katika chuo kingine chochote kile kutosheleza mahitaji ya shahada za kiakademia.

______________________ 18/10/2017

OTUCHI TIMOTHY MALASI Tarehe

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini ya wasimamizi wafuatao walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________ 23rd October 2017

Prof. M.H. ABDULAZIZ Tarehe

(Msimamizi)

______________________ 19/10/2017

DKT. AYUB MUKHWANA Tarehe

(Msimamizi)

# TABARUKU

Kwa wanangu wapendwa Innocent na Natalie. Mlivumilia sana wakati niliposhindwa kucheza nanyi ili nitimize mahitaji ya shahada hii.

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii

TABARUKU ........ iii

YALIYOMO ........ iv

SHUKRANI ........ viii

ISTILAHI NA MANENO MAKUU ........ ix

MAJEDWALI ........ xi

CHATI ........ xii

**SURA YA KWANZA ........ 1**

**LUGHA KATIKA IDARA YA UHAMIAJI NCHINI KENYA ........ 1**

1.1 Usuli wa Mada ........ 1

1.1.1 Lugha kati ya wanaidara na wahudumiwa ........ 1

1.1.2 Lugha baina ya wanaidara ........ 2

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 3

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 3

1.4 Nadharia tete ........ 4

1.5 Sababu za Kuteua Mada ........ 4

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti huu ........ 4

1.7 Yaliyoandikwa kuihusu Mada hii ........ 5

1.8 Msingi wa Kinadharia ........ 8

1.8.1 Nadharia ya Ujumlishaji (Ushirikishi) ........ 8

1.8.2 Nadharia ya msimbo finyu na msimbo pana ........ 10

1.9 Mbinu za Utafiti ........ 14

1.9.1 Sampuli ........ 14

1.9.2 Ukusanyaji data ........ 15

1.9.3 Uchanganuzi wa data ........ 15

**1.10 Hitimisho** .......... 16

**SURA YA PILI** .......... 17

**SAJILI YA MAENEO YA KAZI** .......... 17

2.0 Utangulizi .......... 17

2.1 Sajili .......... 17

2.2 Vipengele vya kutambua sifa za Sajili .......... 19

2.2.1 Msamiati .......... 19

2.2.2 Sentensi .......... 23

2.2.3 Kiimbo .......... 25

2.2.4 Uchanganyaji na uhamishaji msimbo .......... 26

2.2.5 Matumizi ya tamathali .......... 30

2.2.6 Hitimisho .......... 31

**SURA YA TATU** .......... 32

**UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA LUGHA YA IDARA YA UHAMIAJI** .......... 32

3.0 Utangulizi .......... 32

3.1 Uchanganyaji na uhamishaji msimbo katika lugha ya wanaidara na wahudumiwa .......... 32

3.2 Ubadilishaji na uhamishaji msimbo baina ya wanaidara .......... 37

3.3 Hitimisho .......... 39

**SURA YA NNE** .......... 41

**SENTENSI KATIKA LUGHA YA IDARA YA UHAMIAJI** .......... 41

4.0 Utangulizi .......... 41

4.1 Sentensi za Kimuundo kwa Jumla .......... 41

4.2 Sentensi katika Lugha baina ya Wanaidara na Wahudumiwa .......... 44

4.2.1 Sentensi Sahili .......... 44

4.2.2 Sentensi Ambatani .......... 46

4.2.3 Sentensi changamani .......... 48

4.3 Sentensi za lugha baina ya wanaidara ........ 49

4.4 Sehemu za sentensi zilizotumiwa badala ya sentensi nzima ........ 50

4.4.1 Virai ........ 51

4.4.2. Vishazi ........ 53

4.5 Hitimisho ........ 55

**SURA YA TANO ........ 56**

**MUHTASARI, CHANGAMOTO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........ 56**

5.0 Utangulizi ........ 56

5.1 Muhtasari ........ 56

5.2 Muhtasari wa matokeo ........ 58

5.2.1 Ubadilishaji msimbo ........ 58

5.2.2 Sentensi ........ 59

5.3 Changamoto zilizoukabili utafiti huu ........ 59

5.3 Hitimisho ........ 60

5.4 Mapendekezo kwa utafiti wa baadaye ........ 61

**MAREJELEO ........ 62**

**VIAMBATISHO ........ 64**

Kiambatisho cha Kwanza ........ 64

Kiambatisho cha Pili ........ 66

Kiambatisho cha Tatu ........ 67

Kiambatisho cha Nne ........ 70

Kiambatisho cha Tano ........ 73

Kiambatisho cha Sita ........ 77

Kiambatisho cha Saba ........ 77

Kiambatisho cha Nane ........ 77

Kiambatisho cha Tisa ........ 78

Kiambatisho cha Kumi ........ 78

## IKISIRI

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa lugha ya mazungumzo katika Idara ya Uhamiaji nchini Kenya. Ni utafiti uliokuwa na malengo mawili ambayo ni; kubainisha aina za sentensi zinazotumika katika mazungumzo katika Idara ya Uhamiaji; na kubainisha uhamishaji na uchanganyaji msimbo na sababu zake katika Idara ya Uhamiaji. Tulifanya hivi kwa kuzingatia aina na miundo ya sentensi zinazotukia katika matumizi ya lugha baina ya wanaidara wenyewe na baina ya wanaidara hao na wahudumiwa ambao ni jumla ya umma unaokuja kutafuta huduma katika ofisi hizi. Ukiukaji wa kanuni za kisarufi ni wa hali ya juu, sentensi mseto hutumiwa kutegemea mada ya mazungumzo japo nyingi ni sahili na viwango vya uhamishaji na uchanganyaji msimbo ni vya juu vilevile. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili. Nadharia ya ujumlishaji usemi na ile ya Bernstein ya msimbo pana na msimbo finyu. Nadharia hizi ziliteuliwa kutokana na ulinganifu wake kwenye masuala yaliyochunguzwa katika utafiti. Utafiti huu ulibainisha kuwa Idara ya Uhamiaji nchini Kenya husajili uhamishaji na uchanganyaji msimbo pamoja na miundo mbalimbali ya sentensi. Lugha tatu kuu zinazohusika katika uchanganyaji na uhamishaji msimbo ni Kiingereza, Kiswahili na lugha za kienyeji.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao kwa kuchangia pakubwa katika ufanisi wa kazi hii. Kwanza, walezi wangu wa kazi hii ambao walinistahimili licha ya upungufu wangu nilipokuwa nikitekeleza shughuli hii. Hawa ni wasimamizi wangu Profesa Abdulaziz na Daktari Mukhwana. Mwenyezi Mungu awarehemu na kuwabariki ili waweze kukuza wasomi wengine wengi wanaoibukia. Shukrani za dhati pia ni kwa wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Nairobi.

Pili ninatoa shukrani za dhati kwa mke wangu mpendwa Joan Akeyo Otuchi kwa kunihimiza kila nilipohisi kulemewa na kazi hii. Ahsante sana kwa kusimama nami hadi mwisho wa safari hii. Kwa Innocent na Natalie, wanangu wapendwa waliohiari kukosa muda wa kutosha na baba yao ili aweze kuhitimisha kazi hii kwa njia inayostahili. Kwa marafiki zangu wa dhati ambao pia ni wanafunzi wenzangu tulioshiriki nao darasa hili. Hii ndiyo familia ya masomo iliyonipa mahali pa kuita nyumbani wakati wa shughuli hii isiyo rahisi. Hawa ni; Indindi Henry, Gikambi Hezekiel, Biasha Salim, Francisco Gathara, Magara Rita, Kamwanza Rosemary, Dama Rose, Makhulo Evans na Machira Stephen. Ushirikiano wenu na kuhimizana kulichangia pakubwa katika kuitamatisha safari hii.

Idara ya Uhamiaji Mombasa ilinifaa sana katika kazi hii. Kwa maafisa waliokubali kushiriki katika utafiti huu kwa kuniruhusu kuwahoji na hata kujaza hojaji nasema ahsanteni. Hawa ni pamoja na Violet Nasirumbi, Caroline Wamalwa, Ethiophilius Mueke, Maina Gikungu miongoni mwa wengine. Shukrani nyingine ni kwa marafiki wa dhati Jason Opati, Lawi Kwendo na Shem Osomo ambao walikuwa mihimili ya kipekee katika kazi hii. Mungu awazidishie baraka tele.

## ISTILAHI NA MANENO MAKUU

Idara ya uhamiaji – ni idara ya serikali inayotekeleza shughuli za kusajili wananchi, kukagua na kuidhinisha raia wanaosafiri kuingia na kutoka nchini.

Msimbo – tamko lolote kuanzia kwa kiwango kidogo kama cha mofu na mofimu hadi kwenye kauli nzima changamani ya mfumo mzima wa lugha.

Uchanganyaji msimbo – hali ya kutumia lugha mseto katika kiwango cha msamiati katika tukio moja la mawasiliano.

Uhamishaji msimbo – hali ya kutumia lugha mseto katika tukio moja la mawasiliano au diskosi katika kiwango cha vishazi, sentensi au aya.

Wanaidara – wafanyakazi katika idara ya uhamiaji wanaohusika moja kwa moja katika kuwahudumia wananchi wanaokuja kutafuta huduma.

Wahudumiwa – wananchi au watu mbalimbali wanaotembelea idara za uhamiaji kutafuta huduma mbalimbali za idara ya uhamiaji.

# MAJEDWALI

Jedwali 1: Wahudumiwa kwa misingi ya jinsia ........................................................................ 33

Jedwali 2: Msamiati wa Kiingereza katika mazungumzo. ................................................................. 34

Jedwali 3: Msamiati wa Kiingereza kwa misingi ya makundi ya kiumri. ............................................. 36

Jedwali 4: Aina za Sentensi kwa Misingi ya Jinsia. ........................................................................ 43

# CHATI

Chati 1: Msamiati unavyotumika idarani ........................................ 35

Chati 2: Ubadilishaji msimbo kulingana na umri ........................................ 37

# SURA YA KWANZA

# LUGHA KATIKA IDARA YA UHAMIAJI NCHINI KENYA

Katika sura hii tunaelezea msingi wa utafiti wetu kwa kuelezea masuala kama vile usuli wa mada, malengo, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti tutakazotumia kwa utafiti. Tunafanya hivi kwa lengo la kuweka msingi ambao uchambuzi wetu wa data kuhusu uhamishaji msimbo na aina na miundo ya sentensi katika sura za tatu na nne utajikita kwavyo.

## 1.1 Usuli wa Mada

Idara ya Uhamiaji ni moja katika idara za serikali zilizo na shughuli nyingi kutokana na haja nyingi zinazowashughulisha wananchi. Idara hii hivyo basi husajili idadi kubwa ya wananchi kutoka pembe mbalimbali na haja mbalimbali. Wananchi hawa hutumia lugha katika kutafuta huduma hizi. Aidha, wanaidara wenyewe wanaowahudumia nao huwa na lugha iliyo na sifa zenye upekee ambazo tuliziona muhimu kwa utafiti wa kitaalamu. Utafiti huu hivyo ni zao la kichocheo cha uchunguzi wa lugha inavyotumiwa katika mawanda ya utendakazi katika idara hii ya uhamiaji ama baina ya wanaidara wenyewe au wanaidara kwa wahudumiwa ambao ni raia kutoka pembe mbalimbali za nchi wajao kutafuta huduma.

Uchunguzi wa matumizi ya lugha umefanywa katika miktadha mbalimbali ikiwemo sokoni, kazini, kanisani na mahakamani. Tafiti hizi zilitumia nadharia mbalimbali na kufikia mahitimisho mbalimbali. Idara ya uhamiaji sawa na idara nyingine za huduma kwa wananchi inajitokeza kuwa na upekee wa aina fulani katika lugha inayotumiwa huko. Pamoja na kwamba ni mazingira ambamo mtafiti amefanya kazi kwa karibu na kuona haja ya kuchunguzwa kitaaluma kwa lugha inayotumiwa.

### 1.1.1 Lugha kati ya wanaidara na wahudumiwa

Lugha baina ya wanaidara na wahudumiwa ndiyo hujitokeza sana kwa sababu shughuli za idara ni kuwahudumia watu hawa wanaohitaji usaidizi katika huduma mbalimbali. Sifa za lugha

wanayotumia ni dhahiri kwa sababu mtagusano baina yao na wanaidara ndio hujitokeza kwa wingi na ndio msingi wa shughuli za idara hasa. Kwa kuwa kuna majibizano baina yao, tutachunguza sifa za lugha kutoka pande zote mbili. Yaani, tutachunguza lugha inayotumiwa na wahudumu wakiwahudumia wahudumiwa na ile inayotumiwa na wanahudumiwa katika kujibu na kusaka huduma zenyewe. Sentensi fupi fupi na sahili zinatarajiwa kwa sababu hali ya kazi ya wanaidara hawa inawahitaji kuwashughulia watu wengi na hivyo hawawezi kuwa na wakati wa kutosha kwa maelezo marefu na sentensi ndefu za kimzunguko. Aidha, hawa wanatarajiwa pia kutokeza sifa za uhamishaji na uchanganyaji msimbo kutokana na hali kwamba kuna uwili au wingi lugha katika shughuli za idara hii.

### 1.1.2 Lugha baina ya wanaidara

Wanaidara hapa ina maana ya wafanyakazi katika idara ya uhamiaji. Wanaidara hawa hutokeza upekee katika utumizi lugha ambapo baadhi ya sentensi za mawasiliano baina yao huwa fupi sana na zilizoshamiri uchanganyaji na uhamishaji msimbo. Aidha, kutokana na utajiri wa kihistoria kuhusu maana na matumizi ya baadhi ya leksimu, kuna mazoea ya ukiushi wa kanuni za kisarufi kuhusu sentensi. Uchunguzi wa matumizi ya lugha katika idara ya uhamiaji eneo la pwani uliangazia mazungumzo baina ya waombaji pasipoti na maafisa wa idara ya uhamiaji wanaowahudumia. Hili lilifanyika kwa kurekodi baadhi ya mazungumzo haya na kuyachunguza kwa makini.

Ni mazungumzo yatakayobainisha namna lugha inavyotumika katika afisi hii kwa kuhusisha mazungumzo ya watu mbalimbali wanaohudumiwa katika afisi za idara ya uhamiaji. Kwa mfano, ni wakati upi lugha ya Kiingereza, Kiswahili au lugha za asili zitumikapo? Pia mazungumzo baina ya maafisa wa uhamiaji bila kujumuisha waombaji pasipoti yalizingatiwa. Kwa mfano, kuna tofauti namna wanavyotumia lugha wakati wanapotekeleza kazi na wakati

usio wa kazi? Uchunguzi huu ulizingatia umri wa wazungumzaji, kiwango chao cha elimu, jinsia yao na maeneo wanayotoka. Mambo yanayowafanya wazungumzaji hawa kuchanganya msimbo yalishughulisha utafiti huu pia.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu utumizi lugha katika mazingira mbalimbali. Mazingira ya utendakazi ni moja katika sehemu hizi. Hata hivyo, katika asilimia kubwa ya mazingira ya kazi yaliyotafitiwa ni yale ya biashara za masoko huru, sehemu za maabadi miongoni mwa mengine. Tafiti zilizoshughulikia lugha katika mazingira ya kazi hata hivyo nyingi ni za Kiingereza na hizi zilijifunga katika masuala ya mielekeo na matatizo ya mawasiliano katika idara hizi. Aidha, tafiti nyingi zinarejelea lugha ya Kiswahili na hata pale ambapo utafiti umehusu sehemu za kazi katika Kiswahili, mikutadha imejifungia sokoni na sehemu za maabadi kwa kutumia nadharia za diskosi changanuzi tunduizi (CDA) na matendo usemi (Speech Act). Mifano ni Obuchi (2008), Wanjiku (2014) na Kanana (2003). Hakuna utafiti wenye mwelekeo wa kuchunguza masuala ya uhamishaji na uchanganyaji msimbo katika idara ya uhamiaji na vilevile nadharia tulizoteua kwa utafiti huu hazikuwa zimetumikishwa. Utafiti wetu unatumikisha nadharia ya ujumlishi au ushirikishi na ile ya msimbo pana na msimbo finyu. Ni kutokana na mapengo haya ya kitaaluma katika uchunguzi wa lugha katika sekta hii muhimu ambao utafiti wetu unalengwa kushughulikia.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu unaazimia:

(i) Kubaini mikutadha na viwango vya kuchanganya na kuhamisha msimbo katika lugha inayotumiwa katika idara ya uhamiaji nchini Kenya.

(ii) Kubaini aina, miundo na maumbo ya sentensi zinazotumiwa katika mikutadha mbalimbali ya idara ya uhamiaji nchini Kenya.

### 1.4 Nadharia tete

Nadharia tete zinazoongoza utafiti huu ni kwamba:

(i) Kuna viwango vya juu vya uhamishaji msimbo katika lugha inayotumiwa katika idara ya uhamiaji nchini Kenya.

(ii) Sentensi zenye miundo na maumbo mbalimbali yanayokiuka kanuni za kisarufi hudhihirika katika lugha ya idara ya uhamiaji nchini Kenya.

### 1.5 Sababu za Kuteua Mada

Tofauti na tafiti nyingine tangulizi, utafiti huu ulinuia kushughulikia suala la matumizi ya lugha sio tu kwa kuangazia uchanganyaji wa msimbo ambao ni sehemu ya isimujamii mbali pia kwa kuchunguza aina za sentensi zinazojitokeza kwa wingi katika idara ya uhamiaji. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu utachangia pakubwa katika mawanda ya kiusomi kwa kuongeza uelewa wa matumizi ya lugha katika idara ya uhamiaji nchini Kenya. Utafiti huu ni muhimu pia katika kuelewa changamoto zinazojitokeza wakati wa mawasiliano katika idara ya uhamiaji. Suluhisho au njia za kukabili changamoto za mawasiliano katika idara ya uhamiaji zilipendekezwa, jambo ambalo ni muhimu katika uboreshaji wa huduma zinazotolewa na serikali. Hili litawezekana kwa utafiti huu kutoa mwelekeo kuhusiana na masiala kama vile umri, kiwango cha elimu, jinsia na hata maeneo watokayo wale waombaji pasipoti wanaofika pale afisini kuhudumiwa. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwani yanaweza kutumika hata katika idara nyingine tofauti za serikali.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti huu

Nchini Kenya kuna afisi zipatazo tatu zinazoshughulikia maombi ya pasipoti. Afisi hizi hupatikana katika majiji matatu ya nchini Kenya ambayo ni Nairobi, Mombasa na Kisumu. Kwa kuwa Mombasa ni moja kati ya majiji haya matatu, yale yanayolipitikia jiji hili la Mombasa ni yale yale yanayopitikia majiji ya Kisumu na Nairobi. Hivyo basi Mombasa ilikuwa kiwakilishi cha Kenya nzima kama ilivyo Nairobi na Kisumu. Ni kwa misingi hii ambapo tunachukulia

kwamba Mombasa itakuwa ni kiwakilishi tosha cha Kenya nzima hasa katika mahusiko ya lugha inayotumika katika Idara ya Uhamiaji.

Katika utafiti huu, watumiaji lugha ni maafisa wa idara ya uhamiaji, wananchi walioleta maombi ya pasipoti pale idarani, wasaidizi wao pamoja na yeyote aliyefika katika afisi za idara ya uhamiaji kwa nia ya kuhudumiwa. Uchanganyaji na ubadilishaji msimbo katika utafiti huu ulirejelea matumizi ya zaidi ya lugha moja katika mawasiliano. Ni hali inayorejelea matumizi ya zaidi ya lugha moja katika sentensi moja au hata baina ya sentensi tofauti.

Nadharia zilizotumika katika utafiti huu ni Ujumlishaji wa kiusemi iliyoasisiwa na Giles (1975) na ile ya msimbo pana na msimbo finyu ya Bernstein. Mambo yaliyoibuliwa na mihimili ya nadharia hizi yaliingiliana pakubwa na malengo ya utafiti huu. Hivyo, ni nadharia zilizokuwa na mchango mkubwa sana katika utafiti huu.

**1.7 Yaliyoandikwa kuihusu Mada hii**

Labov (1991:183) aliichukulia lugha kama umbo la tabia za kijamii. Mtazamo huu hushikilia kuwa lugha ni tukio la kijamii. Kwa mujibu wa mtazamo huu, lugha haiwezi kutenganishwa na jamii mahsusi. Kuna fafanuzi nyingine nyingi za lugha zikiwemo zile ambazo zinaegemea upande wa isimu nafsia. Mwanaisimu aliye na mtazamo kama huu ni Crystal (1997:214) ambaye aliifasiri lugha kama elementi akilini ambayo hujidhihirisha nje katika mkusanyiko wa sentensi. Mtazamo kama huu unaegemea upande wa isimu nafsia. Mitazamo hii inadhihirisha jinsi ilivyo vigumu kutoa fasiri ya lugha inayofumbata mambo yote yanayohusu lugha. Hata hivyo, jambo moja ambalo wengi wa wanaisimu wanakubaliana nalo ni wazo kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano. Ni bayana kuwa uchunguzi wowote wa lugha huweza kujumuisha maswala mengi na yanayotofautiana.

Akirejelea matumizi ya lugha, Crystal (1959) aliuangalia upungufu wa uelewa wa lugha wa mzungumzaji kama mojawapo ya sababu zinazochangia uchanganyaji wa msimbo. Anaeleza

kuwa mzungumzaji baada ya kushindwa kujieleza vilivyo na kikamilifu katika lugha moja, hubadilisha msimbo ili kuboresha lugha husika na hivyo kueleweka vizuri. Aidha, alirejelea suala la vikundi au makundi katika mchakato mzima wa mawasiliano. Crystal naye alieleza haja ya ushirikiano na kikundi maalum kama jambo lingine lililoathiri namna watu hutumia lugha. Matumizi ya lugha yanaweza kuwa kwa njia ya kuwatenga wengine katika kikundi fulani ambao hawaielewi lugha husika.Utafiti huu ulinuia kubaini iwapo hali hii hujitokeza katika mawasiliano yanayotokea katika afisi za idara ya uhamiaji Mombasa.

Fasold (1957), katika *The Herald online* 2011, alirejelea suala la utambulisho kwa kufafanua kwamba, mzungumzaji anaweza kutaka kuonekana kama mmoja wa watu wenye asilia fulani ya kikundi kisichokuwepo au akataka kujitenga na kikundi fulani na hivyo basi hutumia lugha kwa namna fulani au hata kubadili lugha anayoitumia. Hali hii ndiyo idhihirikayo katika matumizi ya lugha baina ya wanaidara katika idara ya uhamiaji nchini. Wao hutumia lugha katika upekee wake ambao kwa kiwango kikubwa haufungwi na kanuni za kisarufi.

Lugha inaweza pia kuathiriwa na mtazamo wa mzungumzaji kumhusu msikilizaji wake ikiwa ni pamoja na kuwa na uhusiano wa kirafiki, kuchukizwa, kujitenga, kejeli, mzaha, kutilia mkazo na hata kutoridhika. Makala haya yalitoa mwanga zaidi kwa utafiti huu uliochunguza matumizi ya lugha katika idara ya uhamiaji Mombasa. Hii ni kwa sababu uhusiano baina ya wahusika na namna wanavyotumia lugha ni mambo yasiyo ya moja kwa moja na yanastahili kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kueleweka.

Taylor (1976) alirejelea uwililugha kama hali ya mtu kuweza kuzungumza lugha, lahaja au mitindo miwili au zaidi na hii yote inadhihirisha tofauti katika sauti, msamiati na sintaksia. Hali hii husababishwa na ukaribu wa kijiografia na kimaeneo, ndoa, masiala ya kihistoria, uhamiaji, dini, mahusiano ya kitaifa na kimataifa pamoja na sera za lugha.

Hali ya uwililugha huanza wakati mzungumzaji wa lugha moja huweza kutoa kauli kamili na zenye maana katika lugha nyingine. Mawazo haya yanalingana na yale ya Crystal (1975) ambaye anashikilia kuwa uwililugha ni hali ya mtu kuweza kuongea lugha mbili ama kikamilifu au kwa kiasi fulani. Hata hivyo, Bloomfield (1933) anaonekana kutofautiana na wenzake pale anapouona uwililugha kama umilisi kamili wa lugha mbili kama ule alio nao mzawa wa lugha husika.

Uchunguzi wa matumizi ya lugha hasa katika mazungumzo imekuwa mada ya kuvutia katika isimu kwa muda mrefu kwa watafiti. Tafiti nyingi zimechunguza matumizi ya lugha katika diskosi mbalimbali ikiwemo siasa, sheria, mahakamani, falsafa miongoni mwa nyingine.Teresia Wanjiku (2014) alifanya uchunguzi kuhusu matumizi ya lugha katika kanisa katoliki. Utafiti huu ulilenga kuchunguza ubadilishaji wa msimbo katika kanisa Katoliki. Matumizi ya lugha za kilatini, Kiswahili na kiingereza katika mahubiri ni baadhi ya mambo aliyolenga kuchunguza msomi huyu. Mazingira ya utafiti wa Wanjiku yalikuwa kanisa la katoliki. Licha ya kuwepo uhusiano wa utafiti huo na huu, ni bayana kuwa muktadha wa uchunguzi huu ni tofauti kabisa na ule wa kazi ya Teresia.

Kanana (2003) alichunguza matumizi ya lugha katika soko la 'Village market' jijini Nairobi. Utafiti huu ulichunguza namna wauzaji na wanunuzi wanavyotumia lugha wakati wa kununua na kuuza bidhaa mbalimbali katika soko hilo. Uchunguzi huu ulijikita sana katika kuchunguza namna watumizi wa lugha wanavyochanganya msimbo wakati wa kuwasiliana. Utafiti huu ulitumia nadharia ya utambulisho wa kijamii hasa kwa kurejelea mawazo ya Tajfel (1979). Kwa mujibu wa Tajfel, watu hutumia lugha kwa namna inayowahusisha na kundi fulani au kuwatenga na kundi fulani katika jamii. Kazi hii ya Kanana inaweza kulinganishwa na hii kazi yetu, tofauti ikiwa muktadha pekee.

Tajfel (1979) akirejelea suala zima la matumizi ya lugha anashikilia kuwa watu huwa katika makundi mbalimbali tumizi lugha katika jamii na kila kundi hutumia lugha kwa namna inayolitambulisha kundi hilo kutoka kwa makundi mengine. Kwa mfano, kundi la wanafunzi wa chuo kikuu huenda likatumia lugha kwa njia inayolitofautisha na kundi la vijana wa mtaa. Vivyo hivyo, watu wa tabaka la chini huenda likatumia lugha kwa njia iliyo tofauti na litakavyofanya kundi la watu wa tabaka la juu. Hivyo, suala la matumizi ya lugha kwa mujibu wa Tajfel ambaye ni miongoni mwa waasisi wa nadharia ya utambulisho wa kijamii linahusisha lugha na makundi mbalimbali ya watumizi wa lugha.

## 1.8 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeteua kutumia nadharia mbili – nadharia ya ujumlishaji (ushirikishi) na ya msimbo pana na msimbo finyu. Tuliteua kutumia nadharia hizi mbili kutokana na maumbo ya mambo ya tunayotafitia. Tulilitazama suala la uchanganyaji na uhamishaji msimbo kama matukio yaliyowalazimu watumizi lugha kupata mikakati ya kuhusika katika mawasiliano na kufidia upungufu wa aina mbalimbali katika mawasiliano. Nadharia ya msimbo pana na msimbo finyu nayo ilitusaidia kueleza ni vipi ubanaji wa maneno hufanyika katika baadhi ya mikutadha ya utumizi lugha katika Idara ya Uhamiaji.

### 1.8.1 Nadharia ya Ujumlishaji (Ushirikishi)

Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Giles na Street (1975). Nadharia ya ujumlishaji wa kiusemi huchunguza mabadiliko ya kiisimu katika miktadha ya kijamii. Ni nadharia inayotokana na ule msukumo wa kutaka kuelewa uhusiano uliopo baina ya lugha na mabadiliko yatokeayo katika jamii. Nadharia hii hujaribu kufafanua baadhi ya mambo yanayosababisha mabadiliko katika namna ambavyo watu hutumia lugha ya kiusemi katika miktadha tofauti ya kijamii.

Nadharia hii huchangia katika ufafanuzi wa michakato inayosababisha wazungumzaji kuegemea au kuepuka kusema mambo kwa namna fulani.

Mtu anapofaulisha matumizi ya lugha kwa namna iliyo sawa na wengine katika misingi ya matamshi, urefu wa matamko, mpumuo miongoni mwa mengine, basi mtu huyo huwa anadhihirisha hali ya ujumlishaji. Hata hivyo, kuna hali ambapo mzungumzaji hujitenga kabisa na namna wazungumzaji wengine wanavyotumia lugha na huwa hataki kujihusisha na jinsi wenzake waitumiavyo lugha. Hali hii *(divergence)* hubainisha tofauti zilizoko baina ya watumizi mbalimbali wa lugha. Wakati wa maingiliano ya kijamii, washiriki hulazimika kubadili (kujumlisha) jinsi wanavyozungumza kwa lengo la kuafikia mojawapo au hata zaidi ya malengo yafuatayo:

a) Kuibua hali ya kukubalika kijamii hasa kwa wasikilizaji wake. Watumizi wa lugha hutaka kutumia lugha inayokubalika katika jamii na inayochukuliwa kuwa ya hadhi au ya heshima. Hivyo wazungumzaji hujaribu kadri ya uwezo wao kuhakikisha kuwa jinsi wanavyozungumza ni kulingana na matarajio ya jamii.

b) Ili kuwezesha ufanisi katika mawasiliano baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Lengo kuu la mazungumzo ni kufaulisha mawasiliano. Wazungumzaji hujaribu kutumia lugha ambayo haitakwamisha shughuli ya mawasiliano. Kwa hivyo, kwa kutegemea msikilizaji wake, mzungumzaji hutumia lugha anayodhani itafaulisha mawasiliano.

c) Ili kudumisha utambulisho wa kijamii unaokubalika. Kama tulivyotanguliza, mtu ni zao la jamii na kwa hivyo kila mtu hujitahidi sana kutoenda kinyume na matarajio ya jamii yake. Hivyo watu hubadilisha namna wanavyoitumia lugha ili iendane na matarajio ya jamii yake.

Kwa mujibu wa Giles (1975), nadharia ya ujumlishaji wa kiusemi ina msingi wake katika mihimili ifuatayo: Kwanza, watu huwa na ukuruba au hupendelea matumizi ya lugha ambayo huchukuliwa kuwa yanakubalika na wapokezi wao. Mhimili huu pia hushikilia kuwa watu hutumia lugha kwa namna fulani pale panapokuwa na haja ya kueleweka vizuri na kwa njia bora. Nadharia hii pia hushikilia kuwa watu hutumia lugha kwa namna fulani wakati ambapo maadili ya kijamii hayaruhusu njia nyingine ya kutumia lugha katika mazingira kama hayo.

Ukuruba au mwegemeo huu wa namna fulani ya matumizi ya lugha hutegemea mambo mbalimbali kwa mujibu wa nadharia hii ya ujumlishaji wa kiusemi. Kwanza, kiwango cha uelewa cha mzungumzaji au ujuzi wa lugha alio nao mtu. Watu hutumia lugha kulingana na kiwango au ujuzi alio nao mtu. Jambo lingine ambalo huathiri matumizi ya lugha ni tofauti na masuala ya kibinafsi na kimazingira ambayo huchangia hamu ya kutaka kukubalika katika jamii. Uwezo wa hali ya juu wa kujieleza pia huathiri jinsi wazungumzaji mbalimbali wanavyotumia lugha. Watu walio na uwezo wa juu wa kujieleza hufanya hivyo bila ya matatizo yoyote wala kusitasita.

Nadharia ya ujumlishaji wa kiusemi hushikilia kuwa uegemezi wa matumizi ya lugha kwa njia fulani hupokelewa vyema na wapokezi pale ambapo matokeo ya mazungumzo hayo huhusishwa na nia njema. Watu hufurahia mazungumzo yanayohusishwa na nia njema. Mazungumzo hupokelewa vyema pia pale yanapochukuliwa kuwa yenye kuleta utangamano.

### 1.8.2 Nadharia ya msimbo finyu na msimbo pana

Istilahi za msimbo pana na msimbo finyu zimetajwa na Bernstein (1971) katika kazi yake. Kutokana na uchunguzi wake, kila lugha humwezesha mzungumzaji kuwa njia tofauti za kutumia lugha hiyo. Msemaji husemekana kuwa anajimudu katika lugha anapokuwa huru kusema lugha hiyo bila tashwishwi yoyote katika sajili mbalimbali. Yaani haitoshi mtu kujifunza

na kujua kusema lugha tu. Ni lazima ajifunze lugha hiyo kwa mapana na marefu yake. Bernstein (ashatajwa) alifanya uchunguzi wake miongoni mwa wanafunzi kutoka tabaka la kati na wale kutoka tabaka la chini linalojumuisha wafanyikazi wa viwango vya chini. Utafiti wake ulionyesha kuwa mwongeaji anayetalii lugha yake na kudhibiti sajili mbalimbali za kuzungumzia hujimudu kimawasiliano katika miktadha mingi. Mtu kama huyu huwa huru anapoitumia kuliko yule ambaye ameitalii lugha husika kwa kiasi fulani tu. Mtu ambaye amedhibiti mitindo michache ya utaratibu wa mawasiliano mara nyingi hukabiliwa na vikwazo katika kutumia lugha kutokana na ujuzi na tajriba yake finyu.

Kulingana na Bernstein (1971:178) watu hutambua nafasi na maeneo yao katika jamii kutokana na misimbo ya lugha wanayotumia. Msimbo anaotumia mtu huwa kitambulisho chake katika jamii. Kwa maana hii, utumizi lugha wa kuchanganya na kuhamisha msimbo unaweza kuwa kitambulisho cha nafasi ya mtu katika kiwango chake cha elimu, mahusiano au dhima ya mawasiliano. Yaani mtumizi lugha anaweza kutumia iktisadi ya maneno sawa na ilivyo katika iktisadi ya maneno kwa mtu au kundi la watu walio na uhusiano wa karibu, kutokana na uelewa wa mada au haja ya kutopoteza muda mwingi katika tukio hilo la mawasiliano. Matumizi ya sentensi sahili, na vijisehemu vya sentensi ni mifano tu ya misimbo finyu hii katika matumizi. Msimbo finyu hutekeleza kazi kwa kiwango kikubwa katika mazingira ambamo wahusika katika utumizi lugha huo wao uhusiano wa kimsigano na hivyo mawasiliano baina yao hawayapi urasmi mkubwa kama inavyoweza kuwa katika msimbo pana.

Msimbo pana hueleza kila kitu na hili linawezekana tu katika matumizi ya sentensi changamani na kamilifu kimuundo. Kwa hivyo, huku ukiwa msimbo finyu kwa wanaidara kuwasiliana kwa kutumia akronimu kama vile 'BC', 'R number' wakiwasiliana na wanaidara wenzao ambao bila

shaka kutokana na uhusiano baina yao, wataelewana kwa wepesi lakini katika mazingira yayo hayo, mwanaidara akiwasiliana na mhudumiwa ambaye huenda asibaini ukamilifu wa akronimu hizi, atalazimika kutumia maneno kwa ukamilifu yaani msimbo pana ili mhudumiwa aweze kumwelewa kikamilifu. Bernstein (ashatajwa) alisisitiza kwamba msimbo si lahaja.

Upambanuzi kati ya msimbo pana na msimbo finyu unaweza kuelezwa katika kiwango cha isimu kulingana na uwezekano wa kubashiri kutokana na miundo ya kinahau inayotumiwa kupanga na kutoa maana. Katika msimbo pana, mzungumzaji atakuwa na uwanja mpana zaidi wa uteuzi. Hivyo, uwezekano wa kubashiri utaratibu wa kupangia miundo ya sentensi unakuwa haba. Katika msimbo finyu, uwanja wa uteuzi huwa finyu na uwezekano wa kubashiri utaratibu wa miundo nao huongezeka. Katika kiwango cha saikolojia, aina hizi za msimbo zinaweza kubainishwa kulingana na kiasi ambacho kwacho kila moja inakatiza uwezo wa mzungumzaji kuashiria madhumuni kwa uwazi katika kuongea.

Msimbo pana ni wa kiwango cha juu kuliko msimbo finyu na hujitokeza hivi;

(a) Katika kujieleza

(b) Usahihi kisarufi

(c) Uchanganuzi kimantiki

Wazungumzaji wa msimbo finyu hawana eneo pana la kujieleza. Msimbo pana mara nyingi huwa wenye hadhi na hulingana na usanifu wake. Kutumia msimbo pana kutoka utotoni kunaongeza mantiki katika kufikiria. Mathooko, (2007) anaainisha aina tatu za kubadili msimbo ambazo ni kubadili vishinikizo, kubadili msimbo baina ya sentensi na kubadili msimbo ndani ya sentensi.

(a) **Kubadili msimbo vishinikizo.**

Hali hii inatokana na kule kuingiza kirai cha lugha moja kwenye kauli au taarifa iliyo katika lugha nyingine. Ni muhimu kutambua hapa kuwa kishinikizo ni msemo unaonukuliwa mara nyingi na watu. Vishinikizo huingizwa popote kwenye sentensi bila kuvunja sheria za kisintaksia. Mifano ya vishinikizo ni;

"I say"

"You know''

"Yeah''

"Ngai''

"Mwana''

"haya''

"aisee''

"atsi''

**(b) Kubadili msimbo baina ya sentensi**

Huku mi kule kubadili msimbo katika mipaka ya kishazi au sentensi ambapo kishazi au sentensi hiyo huwa katika lugha moja. Kubadili msimbo kwa aina hii huhitaji ufasaha katika lugha mbili zinazohusika kuliko ilivyo katika kubadili vishinikizo kwa sababu sehemu kubwa ya sentensi hiyo sharti ifuate kanuni za lugha zote mbili. Kwa mfano, "*I will repeat please*, ikiwa umeleta mtoto na ana zaidi ya miaka kumi na minane tunakuomba utoke nje.''

**(c) Kubadili msimbo ndani ya sentensi**

Kubadili msimbo ndani ya sentensi kunahusisha msimbo kubadilishwa ndani ya kishazi au sentensi. Aina hii ndiyo hasa hujulikana kama kuchanganya msimbo. Kwa mfano:

*1. Naenda mjini kufanya shopping*

2. *Wanasafiri kwenda gicagi kumtembelea mama.*

Kwa hivyo, badala ya mwanaidara kutumia maneno mengi ya kikanuni katika sentensi kama vile, 'Tafadhali nisaidie na kibanio (*stapler*)' anaweza kupangua baadhi ya hatua hizo za kisarufi na kusema 'kibanio (*stapler*) tafadhali' na ujumbe ule ukawa umemfikia mwanaidara mwenziwe. Huu upunguzaji ama uchumi wa maneno na viambajengo vya sentensi ndio unaokuwa msingi wa nadharia ya iktisadi ya maneno. Mifano hii ya iktisadi ya maneno ilidhihirika pakubwa katika lugha baina ya wanaidara katika idara ya uhamiaji. Kauli za kiisimu zilizotolewa na mzungumzaji huyu hata hivyo sharti ziwe na uwezo wa kufasiriwa kwa maana hiyo katika mfumo pokezi wa mtumizi lugha mwingine.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Huu ni utafiti wa nyanjani. Kwa maana hiyo tutakusanya data ya aina na miundo ya sentensi katika mazingira haya ya utendakazi pamoja na data ya ubadilishaji msimbo.

### 1.9.1 Sampuli

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka kwa watu walioleta maombi ya pasipoti kutoka afisi za idara ya uhamiaji na wanaidara wenyewe kwa wenyewe. Kwa kuzingatia umri, jinsia, kiwango cha elimu na maeneo watokayo washiriki hawa, mazungumzo walioshiriki yalirekodiwa na kuandikwa kwa minajili ya kutumika katika utafiti huu. Washiriki hawa waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampuli wa kimaksudi. Ni mazungumzo haya ndiyo yaliyobainisha aina za sentensi zinazotumika kwa wingi na vilevile namna hali ya uchanganyaji msimbo inavyojitokeza katika mazungumzo hayo. Washiriki hawa walichunguzwa ili kubaini aina za sentensi walizotumia kwa wingi katika mawasiliano yao na vilevile hali za ubadilishaji msimbo katika mawasiliano hayo.

### 1.9.2 Ukusanyaji data

Tulivyodokeza hapo awali, mbinu ya mshiriki-mtazamaji ilitumika sana katika utafiti huu. Mtafiti alijumuika na kuingiliana na maafisa wenzake na wananchi walioleta maombi ya pasipoti bila kuwajuza kuhusu utafiti uliokuwa ukiendelea. Pia mtafiti alishiriki mazungumzo na wote hapo afisini huku akirekodi baadhi ya mazungumzo hayo kisiri. Mazungumzo hayo yalirekodiwa kwa madhumuni ya kutumika katika utafiti huu. Washiriki waliolengwa waliteuliwa kwa misingi ya umri, jinsia, kiwango cha elimu na maeneo watokayo washiriki hao. Mazungumzo baina ya baadhi ya maafisa wa idara ya uhamiaji na waombaji pasipoti pia yalirekodiwa ikiwa ni pamoja na yale yaliyotokea baina tu ya maafisa pekee yao. Kwa kupitia mazungumzo haya, sentensi kama zilivyotumika katika mazungumzo haya zilichunguzwa kwa kuzingatia aina, muundo na uchanganyaji msimbo. Aidha, mifano ya uchanganyaji na uhamishaji msimbo yalichunguzwa katika semi za watumizi lugha hii kwa nia ya kubaini ikiwa ubadilishaji msimbo ulikuwa moja ya sifa bainifu za sajili ya idara ya uhamiaji.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa data

Uchanganuzi wa data iliyokusanywa ulifanywa kwa kutumia utaratibu wa kimsingi wa kuchanganua data. Kwa hivyo, data ilichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi sahili. Uchanganuzi huu ulilenga kupata asilimia zaidi. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuonyeshwa kwa majedwali na pai chati mbali na kutolewa maelezo ya kina.

## 1.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeweka msingi wa utafiti wetu kwa kueleza masuala muhimu kama vile usuli wa mada, malengo ya utafiti, nadharia tete zinazoongoza utafiti huu na upeo na mipaka ya utafiti huu. Aidha, tumeshughulikia msingi wa kinadharia kuhusiana na mada pamoja na kurejelea yaliyoandikwa kuhusiana na mada hii. Isitoshe, tumeeleza mbinu za utafiti tutakazotumia kwa utafiti huu. Tumefanya hivyo kwa lengo la kuweka msingi wa kuongoza maelezo na uchambuzi wetu katika sura za pili, tatu na nne.

# SURA YA PILI

# SAJILI YA MAENEO YA KAZI

## 2.0 Utangulizi

Tasnifu hii inahusu lugha katika muktadha wa idara ya uhamiaji. Idara hii ni moja katika sehemu za utendakazi ambazo kwa kawaida hudhihirisha matumizi ya lugha maalumu na katika mitindo maalumu ya utumizi lugha huo. Idara ya uhamiaji ina aina ya lugha inayoipambanua na kuitofautisha na aina nyingine yoyote ile ya muktadha. Hali hii ndiyo inayoitwa sajili kwa kuwa dhana hii huhusu matumizi ya lugha na wala si watumizi wake. Ni kwa misingi hii ambapo katika sura hii tunatanguliza dhana ya sajili ili kupata msingi imara ambao kwao sura zitakazofuata katika tasnifu hii zitajikita.

## 2.1 Sajili

Dhana ya sajili iliasisiwa na mwanaisimu Halliday katika miaka ya 1960. Alikuwa akifuatilia yale yaliyokuwa yametajwa na watangulizi wake, hasa Firth katika miaka ya 1950. Sajili katika taaluma ya Isimujamii humaanisha kaida na mikondo ya kimawasiliano itumiwayo katika hali na miktadha fulani kwa madhumuni maalum. Hivyo, sajili hujihusiha na jinsi lugha inavyotumika katika miktadha mbalimbali. Kwa hali hiyo, sajili ni ubadilishaji wa utaratibu wa matumizi ya lugha kutegemea namna inavyotumika mbalimbali ya kihali. Haya ni kulingana na Iribemwangi na Mukhwana (2010). Sajili pia huitwa rejista.

Mathooko (2007) anaitazama sajili kama mtindo wa lugha kutegemea muktadha wa kijamii. Sajili pia inaweza kuelezwa kama matumizi ya lugha katika viwango maalum. Kwa mfano, maongezi ya kawaida, sheria, biashara, kandanda, ukulima au teknolojia. Matumizi yanayohusika hutawaliwa na masharti kama cheo, muktadha, umri, mahusiano ya kijamii, hali ya mtu na utamaduni. Ni aina au mitindo mbalimbali ya lugha kulingana na matumizi yake katika

hali za kijamii. Kila sajili hudhihirisha sifa fulani zinazoitofautisha na sajili nyingine. Utafiti huu uliangazia upekee huo kama ulivyojitokeza katika muktadha wa Idara ya Uhamiaji.

Ingawa bado upo mjadala, wanaisimu wengi wanaelekea kukubaliana kwamba sajili hutofautiana kutegemea matumizi ya lugha na wala sio mtu anayeitumia lugha. Yaani mtu mmoja anaweza kuwa na sajili mbalimbali kutegemea na hali ya matumizi ya lugha inavyomtaka kufanya. Ni kutokana na hili jambo ambapo uzungumzaji wa watu wengi utakuwa na ishara za kimsamiati, kisintaksia na kifonolojia kuhusu ngazi zao za kijamii na kiuchumi.

Hata hivyo, mzungumzaji mmoja anaweza kubadili toni, msamiati, miundo ya kisintaksia na mengine kutegemea kile anachokizungumzia. Uzungumzaji huweza kubadili sajili ili kutosheleza shughuli fulani kama vile kuingia kortini, uandishi wa insha, kuhubiri na sajili nyingine. Katika hali hizi zote, sajili husika itajibainisha kisintaksia, kilafudhi, kifonolojia, kimsamiati na kimofolojia. Ifahamike pia kuwa kama dhana ya isimujamii, sajili huweza kutambuliwa kwa kuwa na matumizi ya ishara ambazo si za kiisimu kama vile lugha ya ishara inayojengeka katika lugha ya mwili iliyokubalika na jamii tumizi lugha fulani. Aina ya mavazi na rangi mbalimbali pia huweza kutumika katika mawasiliano.

Crystal (1997) anairejelea sajili kama neno litumiwalo katika isimujamii kuelezea mahusiano baina ya mtindo fulani wa matumizi ya lugha na muktadha wake wa matumizi. Yaani, mitindo mbalimbali ya lugha huwahitajia watumizi wa lugha waitumie katika hali na miktadha Fulani na wala si kotekote. Kwa upande wake, Trudgill (1974) huona sajili kama ihusuyo matumizi ya lugha kutegemea kazi wazifanyazo watu mbalimbali. Hivyo, kazi mbalimbali wazifanyazo watu huwa msingi wa aina ya lugha waitumiayo. Hali hii ndiyo izalishayo dhana za lugha ya wahandisi, wanasheria, polisi, walimu miongoni mwa lugha nyingine. Fasiri hii ina maana kuwa yeyote ajibidiishaye kujua kuhusu sajili atakuwa na nidhamu katika matumizi yake ya lugha.

Mfano ni kuwa mwanafunzi anayeelewa sajili atajua jinsi ya kutofautisha lugha atakayotumia na wanafunzi wenzake anapokutana na mwalimu wake.

### 2.2 Vipengele vya kutambua sifa za Sajili

Katika kutambua sifa za sajili, ni vipengele vya lugha pekee ambavyo hutumiwa tofauti na sehemu nyingine kama fasihi ambazo hujumuisha wahusika na matendo yao. Vipengele vya lugha ni pamoja na aina za sentensi na urefu wa sentensi hizo, kiimbo, msamiati, matumizi ya tamathali miongoni mwa mengine.

#### 2.2.1 Msamiati

Msamiati ni jumla ya maneno ya lugha. Kila eneo huwa na msamiati au istilahi mahususi ambazo zitahusishwa na mazingira hayo ya utumizi lugha. Eneo kama tulivyotaja hapo awali katika mazingira ya sajili hurejelea mada inayozungumziwa au mazingira inamotumiwa lugha. Hivyo, kila uwanja au mada huwa na msamiati wake unaoutofautisha na nyanja zingine. Miongoni mwa maswala yanayotofautisha Nyanja hizi ni msamiati teule unaotofautisha kila uwanja au mada. Ilivyobainika kupitia utafiti huu, msamiati unaotumika katika Idara ya Uhamiaji huweza kugawika katika matapo manne makuu. Makundi haya ni;

(a) Msamiati unaorejelea stakabadhi

(b) Msamiati unaorejelea jamaa na familia

(c) Msamiati unaorejelea taaluma

(d) Msamiati unaorejela teknolojia

Ilivyobainika, mazungumzo katika Idara ya Uhamiaji hasa baina ya maafisa wa Idara na wahudumiwa waliofika kuleta maombi ya pasipoti yalirejelea shughuli ya pasipoti. Mazungumzo haya yalitawaliwa na maswali na maelezo kuhusu mambo na stakabadhi zinazohitajika ili kufaulisha shughuli nzima ya kupata pasipoti kutoka kwa Idara ya Uhamiaji. Wahudumiwa wengi waliofika waliuliza kuhusu nini kinachohitajika ili mtu aweze kupata pasipoti huku

mazungumzo mengi ya maafisa wa Idara ya Uhamiaji yakitawaliwa na maelezo ya matakwa hayo. Hivyo, msamiati uliotawala mazungumzo haya ulikuwa ule ule ukitoa maelezo yale yale na mara nyngi maswali yale yale yakirudiwa na wahudumiwa mbalimbali waliofika kuomba pasipoti. Ndiposa msamiati huu ukagawika katika makundi haya manne.

Lugha katika Idara ya Uhamiaji ilidhihirisha upekee fulani kutokana na kutawaliwa na msamiati uliorejelea stakabadhi mbalimbali zinazohitajika wakati wa kuwasilisha maombi ya pasipoti. Stakabadhi hizi zilielezwa kwa lugha za Kiswahili na vilevile kiingereza. Kuna baadhi ambazo licha ya majina yake kujulikana kwa Kiswahili zilirejelewa kwa lugha ya kiingereza kutokana na mazoea ya matumizi katika lugha hiyo ya kiingereza. Wakati mwingine stakabadhi hizi zilirejelewa kwa kifupi tu kama ilivyotokea wakati wa kurejelea kitambulisho cha kitaifa ambapo mara nyingi kilirejelewa tu kama *ID*, kwa maana ya kitambulisho. Wakati mwingine matumizi ya lugha ya Kiswahili kurejelea baadhi ya stakabadhi yaliwatatanisha baadhi ya wahudumiwa waliofika kuleta maombi ya pasipoti. Hii ilitokana na mazoea ya matumizi ya lugha ya kiingereza kurejelea stakabadhi hizo. Mfano mzuri ni *birth certificate* badala ya cheti cha kuzaliwa. Baadhi ya stakabadhi zilizotajwa kila mara katika mazungumzo ya Idara ya Uhamiaji na hivyo kusaidia kutofautisha sajili hiyo na sajili zingine ni;

a) birth certificate (cheti cha kuzaliwa)

b) death certificate (cheti cha kifo)

c) Identity Card (ID) (kitambulisho)

d) Marriage certificate (cheti cha ndoa)

e) divorce certificate (cheti cha talaka)

f) conversion/ rebersion certificate (cheti cha ubadilishaji hali)

g) baptismal card (kadi ya ubatizo)

h) affidavit (hati kiapo)

i) passport (pasipoti)

j) documents (stakabadhi)

k) Clear copy (nakala safi)

Maneno haya na mengine mengi yanayorejelea stakabadhi yalitawala mazungumzo katika idara ya uhamiaji. Hta hivyo, lugha ya kiingereza ilionekana kutumika sana kuliko lugha ya Kiswahili katika kurejelea stakabadhi hizi. Stakabadhi kama hati kiapo zilirejelewa kila mara kwa lugha ya kiingereza jambo linaloweza kuhusishwa na mazoea ya matumizi ya lugha ya kiingereza kuliko Kiswahili kurejelea stakabadhi hiyo muhimu. Ni muhimu kumaliza sehemu hii kwa kusema kuwa msamiati unaorejelea stakabadhi ni mojawapo wa sifa muhimu zinazoitofautisha sajili ya Idara ya Uhamiaji na sajili nyingine zile. Stakabadhi zilizorejelewa katika mazungumzo haya ni zile zilizohitajika wakati wa kuwasilisha maombi ya pasipoti katika idara ya uhamiaji.

Aina ya pili ya msamiati uliojitokeza kwa wingi katika mazungumzo yaliyofanyika katika afisi za Idara ya Uhamiaji ni ule uliorejelea majina ya watu wa familia, jamaa, ukoo au wale waliokuwa na uhusiano na wahudumiwa waliofika kuleta maombi ya pasipoti. Majina haya yalionekana kuwa na umuhimu wa kipekee hasa wakati wa kudhibitisha ikiwa wale waliofika kuleta maombi ya pasipoti walikuwa wakenya halisi. Maafisa wa idara ya uhamiaji waliwahoji wahudumiwa waliofika afisini kuhusu familia na jamaa zao wa karibu. Baadhi ya wahudumiwa walionekana kupendelea lugha ya Kiswahili katika kurejelea watu hawa huku wengine wakihiari kutumia kiingereza. Hata hivyo, kama ilivyobainika, baadhi ya majina yalirejelewa tu kwa lugha ya kiingereza huku watu wachache sana wakitumia Kiswahili kuyarejelea. Majina haya ni kama cousin, inlaw, step brother miongoni mwa mengine. Kwa ufupi, msamiati uliosheheni majina ya watu wa familia na ukoo ulijitokeza pakubwa katika sajili ya Idara y Uhamiaji, jambo

lililochangia pakubwa katika kuitofautisha na sajili nyingine yoyote ile. Msamiati ufuatao ulijitokeza katika karibu kila mazungumzo baina ya maafisa wa Idara ya uhamiaji na wahudumiwa waliofika kuleta maombi ya pasipoti.

a) father (baba)
b) mother (mama)
c) grandfather (babu)
d) grandmother (nyanya au bibi)
e) uncle (mjomba)
f) aunt (shangazi)
g) cousin (binamu)
h) mother in law (mama mkwe)
i) father in law (baba mkwe)
j) brother (ndugu au kaka)
k) sister (dada)
l) Step brother (ndugu wa kambo)
m) step sister (dada wa kambo)
n) niece (mkoi)

Maneno haya na mengine mengi kama yalivyotumika katika mazungumzo ya Idara ya Uhamiaji yaliipatia sajili hii upekee maalum ulioitofautisha na mazungumzo mengine mbalimbali.

Mbali na msamiati unaorejelea majina ya familia n ule unaorejela stakabadhi mbalimbali, msamiati unaorejelea aina aina za taaluma ulijitokeza kwa wingi katika mazungumzo yaliyotokea katika afisi za Idara ya Uhamiaji. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kila mgeni aliyeleta maombi ya pasipoti alihitajika kujaza sehemu ilyouliza taaluma yake. Ilikuwa vigumu

kurejelea baadhi ya taaluma kwa lugha ya kswahili huku taaluma nyingine zikiwa na msamiati ulioeleweka kwa urahisi kwa lugha ya Kiswahili. Sehemu hii pia iliangazia msamiati uliotumika katika shughuli za Idara ya Uhamiaji pale afisini. Huu ni msamiati ullioeleweka vizuri na wafanyikazi wa Idara ya Uhamiaji kutokana na mazoea yao ya kuutumia kila mara pale afisini. Msamiati huu uliwakanganya wengi wa wahudumiwa waliofika pale afisini kwa kutoelewa moja kwa moja kilichokuwa kikirejelewa. Msamiati huu ulijumuisha maneno mengi yakiwemo haya yaliyoorodheshwa hapa chini:

a) control officer (ofisa mwangalizi)
b) recommend (pendekeza)
c) approve (idhinisha)
d) sign (tia saini)
e) forward (peleka mbele)
f) pend (kwamisha/kwama)
g) track (fuatilia)
h) renewal (stakabadhi/cheti kipya)
i) replacement (stakabadhi/cheti mbadala)
j) mutilated passport (pasipoti iliyoharibiwa)

Inavyodhihirika katika matumizi haya ya msamiati ni wazi kwamba lugha katika Idara ya Uhamiaji ina upekee wa msamiati ambao hauwezi kuhusishwa na mazingira mengine. Baadhi ya istilahi hizi zinaweza kuwa na maana tofauti kabisa katika mikutadha mingine ya utumizi lugha.

### 2.2.2 Sentensi

Sentensi ni tamko la kiisimu linalotumiwa kuwasilisha ujumbe. Katika isimu isoamilifu (*non-functional linguistics*) sentensi ni kitengo cha matini kilicho na neno moja au fungu la maneno yaliyounganishwa katika utaratibu maalumu kuwasilisha ujumbe. Hujumuisha kiima cha diskosi

hiyo pamoja na kauli ya ujumbe unaowasilishwa. Sentensi hutuelekeza kuhusu mpangilio au ruwaza ya jinsi ya kuwasilisha mawazo yetu ama katika maandishi au katika matamshi. Kwa kawaida, sentensi kamilifu hujumuisha kitenzi, ambacho huwasilisha wazo kamili na huwa na fahiwa inayoweza kufasiriwa au kujisimamia. Sentensi inaweza kutumia kishazi kimoja huru au kujumuisha vishazi huru na tegemezi. Sentensi ya kutumia vishazi tegemezi sharti iviambatanishe na vishazi tegemezi ndipo kauli inayokusudiwa kuwasilishwa itokezwe kwa ukamilifu.

Sentensi ya kawaida hutimiza mambo haya mawili – huwa na usarufi na ukubalifu. Usarufi ni hali ya kuzingatia kanuni za kisarufi kama vile mpangilio, kiimbo, uakifishaji miongoni mwa mengine. Ukubalifu nao ni zao la uwezekano wa kauli inayowasilishwa na sentensi hiyo kuwa na mantiki na kuweza kupokelewa katika njia iliyokusudiwa na mtoaji wa sentensi yenyewe. Ni kigezo hik cha ukubalifu ambacho waminimalisti hutimiza kwa kupunguza maneno na miundo ya sentensi na kuwasilisha sentensi. Hata hivyo, wazo kwamba sentensi ni kauli kamili linahitaji kwamba sentensi iwe na sehemu hizi mbili – kiima na kiarifu. Sehemu nyingine za sentensi kama kirai, shamirisho na chagizo huwa viambata tu vya kukamilisha sehemu hizi mbili kuu za sentensi.

Uwezo wa kutunga sentensi ni zao la mchakato wa kiakili na tajiriba za utumizi lugha na utamaduni wa mtumizi lugha husika. Utamaduni wa mtumizi lugha hapa haumaanishi ule wa lugha yake ya kwanza pekee bali mazingira mengine ya lugha anazozipata, kujifunza na kuzitumia muda baada ya muda. Tulivyotaja awali katika sehemu hii, ni hali hii ya sentensi kuafiki vigezo vya jamii tumizi lugha ndipo tunapoweza kusema kwamba sentensi hiyo imetimiza ukubalifu wa kisarufi na kimantiki.

Katika kuainisha sifa za sajili, sentensi hurejelewa katika mikumbo miwili – urefu na aina. Kwa maana hii, kuna baadhi ya mazingira ya utumizi lugha ambamo sentensi ndefu ndefu hujitokeza kwa wingi na mengine ambayo sentensi zake ni fupi. Aidha, kuna mazingira ambamo utumizi lugha utadhihirisha sentensi nyingi sahili huku kwingine kukiwa na mzo wa sentensi changamani. Tofauti hizi hutegemea mada inayoangaziwa na haja ya mazingatio ya wakati wa kuzitumia sentensi hizi. Mazingira yanayotumia lugha ya kirejelezi kama vile mahakamani yatakuwa na sentensi ndefu na changamani nyingi ikilinganishwa na mazingira mengine kama ya sajili ya maabadini. Kwa maana hii, iktisadi ya maneno au ubanaji wa maneno katika sentensi unaweza kujitokeza katika sajili mbalimbali za lugha sawa na inavyojitokeza katika lugha ya Idara hii ya Uhamiaji.

Lugha inayotumiwa katika Idara ya Uhamiaji inadhihirisha sifa hizi za sentensi – iktisadi ya maneno ambayo inahusisha matumizi ya virai pekee, maneno tu na vilevile sentensi za kimuundo. Wakati mwingine kutokana na haja ya kuzingatia wakati ili kuwahudumia watu wengi, wanaidara wanaweza kutumia hata vipande au sehemu za sentensi pekee kuwasilisha ujumbe. Yaani kwa mfano, mtu anapotaka huduma ataulizwa '*ID*' bila lazima ya kutunga sentensi kamili. Katika hali nyingine, kauli hizi zinaweza kuwa ndefu kutegemea maelezo anayopewa au anayotoa mhudumiwa.

### 2.2.3 Kiimbo

Kiimbo ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa kuitamka sentensi. Kwa hivyo, kiimbo ni mchakato unaohusu sentensi hivyo huelekeza kuhusu matamshi ya sentensi ikiwa kwa mfano ni kauli ya taaifa au swali; huelekeza kuhusu sentensi hiyo itakavyoakifishwa; huelekeza kuhusu kasi ya kuitoa sentensi na wakaa wa kupumzika katika hatua mbalimbali za utamkaji wa sentensi hiyo. Kwa maana hii, kiimbo kinaweza kuwa cha haraka au cha taratibu kutegemea mazingira au mada ya utumizi lugha.

Kuna mazingira ya utumizi lugha ambayo huhitaji kiimbo cha haraka cha mawasiliano na mengine yasiyohitaji kiimbo hicho. Kwa maana hii, lugha ya kutangaza mchezo kama vile kandanda haiwezi kuwasilishwa kwa kiimbo sawa na kile cha lugha inayotumiwa kuwasilisha kesi au suala mahakamani. Kiimbo cha lugha huelekezwa hivyo basi na mazingira ya utumizi lugha au mada inayowasilishwa. Mtumizi lugha aliyekasirishwa na anayetokeza hisia zake kutokana na suala lililomuudhi anatarajiwa kutumia lugha kwa kiimbo cha haraka kutokana na hali hiyo aliyomo tofauti kabisa na mtu yuyo huyo akiwa katika hali na mazingira tulivu.

### 2.2.4 Uchanganyaji na uhamishaji msimbo

Ingawa dhana hizi mbili zimetofautishwa, katika utafiti huu, dhana hizi zilielezwa au kurejelewa kama dhana moja tu ya kutumia aina mbili za msimbo katika matini moja wakati wa mawasiliano. Dhana ya kubadili msimbo ni dhana inayochunguzwa na wanaisimujamii na isimu nfsia. Wanaeleza kuwa kuna uhusiano mkubwa na wa moja kwa moja kati ya uteuzi wa lugha na muktadha wa kijamii. Katika isimujamii, wachunguzi huangalia sababu ya mtu kubadilisha msimbo. Katika kiwango cha isimu nafsia, ule uwezo unaomfanya mtu kuchanganya na kubadili msimbo ndio unaochunguzwa. Baadhi ya watu wamechukulia kubadili msimbo kama ishara ya kuoza kwa ule uwezo wa kiisimu. Wanaona kwamba kubadili msimbo ni matokeo ya kutojua lugha moja vilivyo. Kiisimu hatuwezi kusema hivyo kwa sababu kule kubadili msimbo ni sifa muhimu katika usemi wowote unaohusu uwililugha. Ni mkakati wazungumzaji wanaotumia katika mazungumzo kwa sababu moja au nyingine.

Uhamishaji na uchanganyaji msimbo ni sifa muhimu zinazochunguzwa katika jamii za wingi lugha. Msimbo ni tamko linalotumiwa mara nyingi kwa maana ya lugha, lahaja au mitindo ya lugha (Gardner-Chloros, 2009:11). Uhamishaji na uchanganyaji nao kwa upande mwingine ni hali za kubadilibadili baina ya lugha mbili au zaidi katika tukio moja la mawasiliano. Wataalamu wengi wamejaribu kujeleza masuala haya ya kuchanganya na kuhamisha msimbo. Hawa ni

pamoja na Amuda (1989), Atoye (1994), Belly (1976) na Ayeomoni (2006). Kwa mfano kulingana na Ayeomoni (2006), Hymes (1974) aneleza uhamishaji msimbo kama "tamko la kawaida la kuelezea utumizi wa lugha au mitindo mbadala mbili au zaidi katika tukio moja la mawasiliano' huku Bokamba (1989) akiieleza dhana hii 'Uhamishaji msimbo ni uchanganyaji wa maneno, virai na sentensi kutoka mifumo miwili tofauti ya kisarufi katika tukio moja la mawasiliano'. Bokamba (1989) anaueleza uchanganyaji msimbo kama 'tukio la kujumuisha vitengo vingine vya kiisimu kama vile viambishi, maneno katika tamko kwa lengo la kueleweshaʼ. Uhamishaji msimbo nao unaelezwa na Gumperz (1982:59) kama "mabadiliko katika tukio moja la mazungumzo ambapo kuna mabadiliko katika aya kutokana na matumizi ya mifumo miwili au zaidi ya lugha".

Utumizi lugha wa kuchanganya au kuhamisha msimbo unaweza kuwa wa kimakusudi au ukajitokeza bila mtumizi lugha mwenyewe kutarajia. Katika utafiti huu tunaufungia uchanganyaji msimbo katika kiwango cha neno au leksimu na uhamishaji msimbo kupanuka hadi katika kiwango sentensi na aya.

Ni muhimu kubaini hapa kwamba miundo ya kisemantiki katika matukio haya uchanganyaji na uhamishaji ni tofauti na diglosia iliyoelezwa na Ferguson (1972), ambapo matumizi ya lugha au misimbo miwili huwa na uamilifu mahsusi katika muktadha huo unaoitumikisha. Ingawa kuna kufanana kwa vipengele vya diglosia na uhamishaji msimbo kutokana na hali kwamba ni lazima mtumizi lugha huyo awe na uwezo wa misimbo yote miwili, diglosia hurejelea uhusiano wa moja kwa moja kati misimbo miwili, huku uhamishaji msimbo ukiitazama sentensi pamoja na mazungumzo inamotukia.

Kuchanganya na kuhamisha msimbo ni sifa zinazoutambulisha mfumo wowote wa jamii zenye uwili-lugha au wingi lugha duniani. Ni michakato inayoweza kumaanisha mambo mengi tofauti

tofauti kwa wataalamu mbalimbali. Watafiti wengi waliochunguza suala hili la uhamishaji msimbo wamejikita fasili za kisosholojia na matumizi ya diskosi hiyo. Hili linaweza kuifanya tasnia ya uchunguzi wa uhamishaji msimbo kuchukulia kwamba ni tukio la kisosholojia tu na hivyo kuifungia katika masuala ya isimujamii pekee. Hata hivyo, mtazamo mpana kuhusu mazingira ambamo mtumizi lugha huteua kuchanganya au kuhamisha msimbo yanaweza kupanua tasnia hii ya utafiti wa kiisimu hadi katika pragmatiki. Kwa hivyo, uchanganyaji na uhamishaji huu msimbo unaweza hata kuwa suala la mapendeleo ya lugha hivyo basi kuonesha mielekeo ya watumizi lugha kuhusu lugha mbalimbali (Auer (mha.) 1998).

Clyne (1991: 193) anaeleza kuwa "maneno katika makutano au njia panda za mifumo miwli ya lugha yanaweza kumsababishia mtumizi lugha kubadili mkondo wa utumizi lugha na hivyo kuendelea kutumia mkondo wa mfumo mmoja wa lugha". Yaani mtumizi lugha anapokuwa na ufahamu wa lugha mbili na anazitumia mahali fulani kwa kuchanganya hali ya kutoweza kuupata kwa haraka msamaiti wa lugha ya kunaweza kumsababishia kuendelea na lugha nyingine aliyokuwa ameanza kuitumia. Uhamishaji msimbo katika kiwango hiki hivyo utakuwa mchakato wa kiakili. Clyne (2003:162) anaongeza kuwa ni muhimu kusisitiza kwamba aina hizo za leksimu zinazomsababishia mtumizi lugha kubadili na kuhamia katika lugha moja hazipaswi kuchukuliwa kama tokeo bali sababu ya uhamishaji msimbo wenyewe. Kwa wanaisimu ya kiakili (*psycholinguists*) hata hivyo neno linalohamishiwa katika lugha nyingine halitatazamwa kama kitengo kilichobadilishwa kwa sababu lenyewe ni sehemu ya mawasiliano hayo.

Uhamishaji na uchanganyaji msimbo unaweza kufanyika katika kiwango chochote cha muundo wa kiisimu, hata hivyo utukiaji wake katika kiwango cha sentensi, neno ndio utakaotushughulisha katika utafiti huu. Moja katika masuala ya kuchunguzwa kuhusiana na uhamishaji na uchanganyaji msimbo ni kuhusu sababu za utukiaji wake. Pana haja ya

kuchunguza sababu za tabia hiyo katika watumizi lugha wenye uwili-lugha na wingi lugha. Hii ndiyo ya sababu ya Gumperz (1982), kueleza kwamba kuna aina hizi mbili za uhamishaji na uchanganyaji msimbo:

- Uhamishaji kutokana na hali *(Situational switching)*
- Uhamishaji wa Kisitiari *(Metaphorical switching)*

Kulingana na Gumpers (ashatajwa) uhamishaji msimbo kutokana na hali huongozwa na hali aliyomo mtumizi lugha ambapo yeye hutumia msimbo mmoja katika hali fulani na mwingine akiwa katika hali nyingine. Kughafilika katika msamiati ni mfano wa hali. Katika uhamishaji wa kisitiari kwa upande mwingine mada ya mazungumzo ndiyo huelekeza lugha itakayotumiwa kwa hivyo mtumizi lugha anaweza kutumia lugha tofauti akiwasilisha mada mbalimbali. Aidha, Gumpers anaongeza kuwa uhusiano baina ya lugha na mazingira ya utumizi wake ni changamani sana hivi kwamba 'wahusika waliozama katika mazungumzo hayo hukosa kubaini ni msimbo gani waliotumia wakati gani' (Gumperz 1982:61). Japo tunakubaliana kwa asilimia kubwa na madai haya ya Gumpers, wakati mwingine watumizi lugha hawa hujua wanapohamisha msimbo kwa sababu wakati huo uhamishaji huu huwa tukio la kimakusudi. Myers-Scotton (1993:75) anampinga Gumpers kwa kudai kuwa wazungumzaji hujua kabisa wakati wanapobadili msimbo. Sisi hata hivyo tunashikilia kuwa mtumizi lugha hujua tu anapobadili msimbo ikiwa analifanya hilo kimakusudi kama vile kwa kukosa kujua au kupata kwa haraka msamiati linganifu kwa neno hilo la lugha anayohamia.

Kulingana na Auer (1998:1-4) uhamishaji msimbo ni sehemu tu ya hatua ya matamshi kama kitengo cha mawasiliano na kutekeleza majukumu ya kijamii vilevile. Kwa hivyo, uhamishaji msimbo hutumiwa kupanga mazungumzo kwa kuchangia maana ya kiuhusiano kwa tamko lililotolewa. Yaani, kulingana naye kuna uhusiano mwema zaidi kwa kuwa watumizi lugha hawa

wanaochanganya na kuhamisha msimbo wana ufahamu mpana kuhusu tukio la mazungumzo wanayofanya au kipengele wanachozungumzia katika tamaduni na mikutadha tofauti na huo mmoja waliomo.

Lugha baina ya wanaidara na katika idara ya uhamiaji kwa jumla, inadhihirisha viwango vya juu kabisa vya uhamishaji na uchanganyaji msimbo. Hivi ni kwa sababu mazingira ya utendakazi katika idara hii huwakutanisha watumizi lugha ambao ama wana usuli wa wingi-lugha au uwili-lugha. Hali hii hujitokeza kwa wote – wanaidara na wahudumiwa. Katika sura ya tatu, mifano ya jinsi uchanganyaji na uhamishaji msimbo inavyojitokeza katika mawasiliano kwenye idara ya uhamiaji yatakuwa bayana. Watumizi lugha katika mazingira haya hubadilisha na kuhamisha msimbo ama kwa kujua kutokana na kutopata msamiati wa lugha hiyo nyingine au kimakusudi kutokana na uwezo wao lugha zote. Yaani, mhudumu au mwanaidara anapomwambia mwenziwe 'nisaidie na *stapler please*' pana uwezekano kwamba hajui msamiati wa 'stapler' katika Kiswahili lakini pia pana uwezekano kwamba ameendelea na neno '*please*' badala ya 'tafadhali' kutokana na athari za kuhamia katika mfumo mwingine wa lugha alipotaja neno '*stapler*'.

### 2.2.5 Matumizi ya tamathali

Lugha ya kitamathali si lugha inayopatikana katika mazingira yote ya utumizi lugha. Lugha hii hutumiwa tu katika mazingira yaliyo na nafasi ya kufasiriwa kwa maana fiche zinazowasilishwa katika tamathali hizo. Lugha ya tamathali tunayorejelea hapa ni lugha inayoshirikisha utumizi wa semi kama vile methali, misemo, nahau, misimbo na lugha nyingine za kimafumbo. Lugha hii ya kimafumbo hutumiwa panapokuwa na haja ya kufumba au kuficha baadhi ya ujumbe ili usiwe wazi kwa wahusika katika mazingira hayo ya mawasiliano ambao hawahusiki moja kwa moja katika suala lenyewe linalorejelewa. Hata hivyo, kwa kiwango kikubwa lugha katika idara ya uhamiaji inatarajiwa kuwa na uwazi au kuwa ya moja kwa moja.

Lugha katika idara ya uhamiaji inaweza kudhihirisha maumbo mawili ya utumizi lugha huu. Mawasiliano baina ya wanaidara yanaweza kushirikisha misimbo inayolenga kuufumba ujumbe kuhusu wahudumiwa panapokuwa na haja ya kushauriana kuhusu hali mbalimbali za kesi zinazoletwa na wahudumiwa hao. Hivyo basi, uwezekano uliopo ni baina ya wanaidara tu kutumia tamathali hizo. Kwa upande mwingine haitatarajiwa mfanyakazi wa idara kutumia lugha ya kimafumbo kwa kiwango kikubwa akiwasiliana na mhudumiwa ila pale ambapo mhudumiwa mwenyewe anaona haja ya kufumba baadhi ya ujumbe akiwasiliana na mwanaidara mwenziwe au mhudumiwa kwa nia ya kuuficha ujumbe usieleweke na wahudumiwa wengine. Kwa mfano wanaidara wanapoliita ombi fulani la pasipoti kuwa *Hajj applications* ni wao wanaoelewa kwamba aina hii ya pasipoti inatumiwa katika mikutadha na mazingira mahususi ya safari ya kuhiji Makka na wala aliyepewa pasipoti hiyo hawezi kuitumia katika shughuli nyingine tofauti.

### 2.2.6 Hitimisho

Ilivyodhihirika katika maelezo ya sura hii, kuna vipengele mbalimbali vya lugha vinavyoweza kutumiwa kuainisha sifa za sajili fulani ya lugha. Katika utafiti huu, tumeteua kushughulikia vipengele viwili ambavyo ni sentensi na msamiati. Tumevishughulikia vipengele hivi kwa kutathmini aina za sentensi zilizotumiwa na mazingira ya utukiaji wake; sehemu za sentensi ambazo kwa haja ya iktisadi au uchumi wa mawasiliano hutumiwa mara kwa mara; na vilevile mazingira ya uhamishaji na uchanganyaji msimbo.

# SURA YA TATU

# UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA LUGHA YA IDARA YA UHAMIAJI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tunachunguza ubadilishaji msimbo unavyojitokeza katika matukio mbalimbali ya utumizi lugha katika Idara ya Uhamiaji mjini Mombasa. Ubadilishaji msimbo tunaorejelea hapa unajumuisha uchanganyaji na uhamishaji msimbo. Kwa kurejelea mifano mbalimbali ya utukiaji wa hali hizi, tumechambua na kutathmini mazingira ambamo hali hizi hutukia.

## 3.1 Uchanganyaji na uhamishaji msimbo katika lugha ya wanaidara na wahudumiwa

Uhamishaji na uchanganyaji msimbo ulidhihirika kwa kiwango kikubwa katika mazungumzo baina ya wanaidara na wahudumiwa. Huku wanaidara wengi wakibadili na kuhamisha msimbo kwa kiwango kukubwa katika mikutadha ya kurejelea stakabadhi na baadhi ya nyaraka muhimu walizohitaji kutoka kwa wahudumiwa, asilimia kubwa ya wahudumiwa walibadili na kuhamisha msimbo wakati mwingi hata katika kujieleza. Asilimia kubwa hata hivyo ya ubadilishaji msimbo ulikuwa kutoka Kiswahili hadi Kiingereza na aghalabu hali hii inajitokeza katika wahudumiwa waliopata elimu ya shule ya upili na zaidi. Aidha, kwa kuzingatia kipengele cha jinsia, inaonekana wazi kuwa wanawake ndio wanaochanganya msimbo zaidi kuliko wenzao wa kiume. Walakini hali hii ilijitokeza sana miongoni mwa wale wanawake ambao wako chini ya miaka thelathini na tano.

Kuanzia miaka thelathini na mitano kuendelea, mkondo ulibadilika na wanaume wakaonekana kuchanganya msimbo kuwaliko wenzao wa kike. Kuna uwezekano kuwa hali hii ilichangiwa na idadi kubwa ya wanawake wanaosoma siku za hivi karibuni ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka ya hapo nyuma. Hii ni kwa sababu idadi kubwa ya wanawake waliochanganya msimbo ni wanafunzi wa shule au vyuo au wale walioajiriwa juzi. Licha ya kuwa wanaume wengi pia huchanganya msimbo katika kundi hili la kiumri, ukweli ni kuwa idadi ya wanawake

waliochanganya msimbo imepiku ile ya wanaume. Hata hivyo, hali hii ilibadilika tulipoangazia makundi ya umri wa miaka thelathini na tano na zaidi ambapo idadi ya wanaume waliochanganya msimbo ilizidi ile ya wanawake. Hali hii iliendelea hivyo hadi umri wa juu zaidi uliochunguzwa katika utafiti huu.

Inavyoonekana pia ni kwamba watu wa jinsia ya kike ndio waliojitokeza zaidi kuomba pasipoti za kusafiria kuliko wale wa jinsia ya kiume. Wengi katika hawa ni wale ambao husafiri ili kwenda kuwaona waume zao wanaofanya kazi katika mataifa ya kigeni. Vilevile, kuna kundi la wanawake walioomba vyeti vya kusafiri ili kwenda mashariki ya kati kufanya kazi kama vijakazi katika nyumba za mabwanyenye na wafanyikazi wa kampuni mbalimbali. Ukweli wa madai haya unadhihirika kupitia jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Wahudumiwa kwa misingi ya jinsia**

| Umri | Wanawake | Wanaume | Jumla | |
|---|---|---|---|---|
| 15-24 | 35 | 23 | 58 | |
| 25-34 | 28 | 12 | 40 | |
| 35-44 | 9 | 20 | 29 | |
| 45-54 | 7 | 13 | 20 | |
| 55-64 | 5 | 8 | 13 | |
| 65 + | 3 | 5 | 8 | |

Utafiti huu ulibaini kuwa mazungumzo mengi yanayofanyika katika afisi za idara ya uhamiaji huhusisha hali ya kuchanganya msimbo kwa wingi. Wengi wa watumizi wa lugha huchanganya msimbo kati ya sentensi na baina ya sentensi. Msamiati wa Kiingereza na Kiswahili hubadilishana nafasi katika mazungumzo haya. Kupitia utafiti huu, ilibainika kuwa wengi wa wanaochanganya msimbo ni wazungumzaji walio na uelewa wa lugha mbili au zaidi. Wengi wa

hawa ni wale waliosoma hadi kiwango fulani na kwa kuchanganya msimbo, huwa wanajitambulisha kwa namna fulani ya kipekee. Kipengele cha elimu kwa hivyo ni miongoni mwa vipengele vilivyotumika katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu.

Utafiti huu ulibainisha kuwa msamiati unaochanganywa katika mazungumzo hutokana na majina ya vifaa vinavyotumika pale kazini, majina yanayorejelea uhusiano wa kiukoo na kurejelea watu wa familia na majina yanayotokana na maendeleo ya kiteknolojia. Zingatia jedwali lifuatalo lenye baadhi ya maneno yanayojitokeza kwa wingi katika mazungumzo yanayochanganya lugha ya kiingereza na Kiswahili.


**Jedwali 2: Msamiati wa Kiingereza katika mazungumzo.**

| MSAMIATI | STAKABADHI | TEKNOLOJIA | TAALUMA | JAMAA |
|---|---|---|---|---|
| | Birth certificate | Download | Control officer | Brother |
| | Death certificate | Upload photo | Recommend | Mother |
| | Identity card (ID) | Cyber | Approve | Father |
| | Marriage certificate | Network | Sign | Uncle |
| | Divorce certificate | Hang | Forward | Aunt |
| | Conversion certificate | Photocopy | Pend | Inlaw |
| | Baptismal card | Browse | Track | Grandmother |
| | Affidavit | Print | Renewal | Sister |
| | Passport | Printout | Replacement | Cousin |
| | Documents | Invoice | Mutilated | |
| | Clear copy | | | |

Kwa ujumla maneno ya kiingereza yote yaliyotumika yalikuwa chini ya matapo haya manne yaliyoorodheshwa katika jedwali hapo juu. Ufuatao ni mgao kwa asilimia wa jinsi maneno ya

kiingereza yalivyotumika kwa kuzingatia matapo hayo. Kati ya maneno mia moja ya Kiingereza yaliyochunguzwa, ifuatavyo ni namna matapo haya yalichangia maneno hayo.

Stakabadhi -28%
Teknolojia -21%
Taaluma -24%
Familia -20%
Mengine -7%




**Chati 1: Msamiati unavyotumika idarani**


Inavyoonekana hapa maneno yanayorejelea stakabadhi zinazohitajika wakati wa kuleta maombi ya pasipoti ndiyo yanayojitokeza kwa wingi zaidi katika lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na yale yanayorejelea familia, taaluma na ya kiteknolojia. Kati ya jumla ya maneno mia moja yaliyochunguzwa, jumla ya maneno ishirini na nane yalirejelea stakabadhi mbalimbali. Hii ni asilimia ishirini na nane ya maneno yote yaliyochunguzwa. (28%) Msamiati wa kitaaluma unaotumika pale idarani kwa lugha ya kiingereza ulikuwa asilimia ishirini na nne (24%) huku msamiati wa kiteknolojia ukichangia asilimia ishirini na moja (21%). Maneno yanayorejelea watu wa familia au ukoo yalichangia asilimia ishirini (20%).

Mbali na matapo haya manne yaliyorejelewa, maneno mengine yasiyopatikana chini ya makundi haya pia yameweza kutumika. Baadhi ya maneno haya yanarejelea sehemu na hali tofauti. Msamiati huu umechangia asilimia saba (7%) ya msamiati uliohusishwa katika utafiti huu.

Kwa kuzingatia kigezo cha kiwango cha elimu, wazungumzaji waliopendelea kutumia msamiati wa Kiingereza katika mazungumzo yao ni wale ambao walikuwa wamesoma hadi kiwango cha shule ya upili na zaidi tulivyosema hapo awali. Waombaji pasipoti ambao hawajahudhuria shule walitumia lugha ya Kiswahili bila ya kuchanganya na Kiingereza. Wengi wa wale waliochanganya msimbo kwa kubadilisha Kiswahili na kiingereza walifanya hivyo kwa nia ya kutaka kujihusisha na kundi fulani la watu ambao ni wasomi. Wazungumzaji wa umri wa kuanzia miaka kumi na sita hivi hadi miaka arobaini na tano hivi ndio waliochanganya Kiswahili na kiingereza zaidi katika mazungumzo yao. Jedwali linalofuata ni la msamiati wa kiingereza jinsi ulivyojitokeza katika mazungumzo kwa misingi ya makundi ya kiumri.

**Jedwali 3: Msamiati wa Kiingereza kwa misingi ya makundi ya kiumri.**

| Umri | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|---|---|---|---|
| 15-24 | 35 | 23 | 58 |
| 25-34 | 28 | 12 | 40 |
| 35-44 | 20 | 9 | 29 |
| 45-54 | 7 | 13 | 20 |
| 55-64 | 6 | 11 | 17 |
| 65 + | 3 | 7 | 10 |




**Chati 2: Ubadilishaji msimbo kulingana na umri**

Kama inavyojitokeza katika jedwali hili, utafiti huu ulibainisha kuwa wazungumzaji wengi wanaochanganya msimbo ni wale wa makundi ya kiumri wa kati ya miaka kumi na tano (15) na miaka arobaini na nne. Kama ilivyobainika kupitia utafiti huu, wengi wa wazungumzaji katika makundi haya ya kiumri wamesoma katika viwango vyote kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu.

### 3.2 Ubadilishaji na uhamishaji msimbo baina ya wanaidara

Lugha baina ya wanaidara wenyewe kwa wenyewe nayo kwa kiwango fulani inadhihirisha uchanganyaji na msimbo. Kauli za wanaidara hawa mara nyingi zilijitokeza wakija kwa ghafla kuomba kifaa fulani cha kazi au wakitaka kubainisha na kuelekezwa kuhusu jambo fulani. Kwa kuwa asilimia kubwa ya wanaidara hawa ina elimu ya zaidi ya shule ya upili, uhamamishaji wa Kiingereza na Kiswahili ni wa kiwango cha juu. Pamoja na hali hii ya elimu, uhamishaji na uchanganyaji wa msimbo ulijitokeza sana katika kuombana vifaa vya kazi na fomu mbalimbali walizohitaji. Aidha, kulidhihirika uhamishaji na ubadilishaji msimbo katika kuelekezana kushughulikia shughuli mbalimbali au maelekezo mbalimbali ambayo wanaidara hawa walishauriana kuwaelekezea wahudumiwa. Kwa mfano, pale ambapo mwanaidara alihitaji

kupunguzwa kwa idadi ya wahudumiwa wa kuruhusiwa kuwa ukumbini kwa wakati mmoja, maelekezo na maagizo ya kuwatoa nje hao wengine wa ziada yalitolewa katika uhamishaji msimbo.

Mazungumzo baina ya wanaidara hudhirihika katika mikumbo mbalimbali. Yapo mazungumzo baina yao wakiwa nje ya mazingira ya kazi na mazungumzo yanayoendelea wakati wanaopokuwa wakifanya shughuli za kuwahudumia wahudumiwa. Mazungumzo yaliyoshughulikiwa hapa ni yale ya wanaidara baina yao wakishauriana kuhusu masuala mbalimbali katika utendakazi wao. Kwa maana hii, mazungumzo haya hayatarajiwi kuwa marefu bali ni mafupi tu lakini yaliyo na utajiri wa data ya kiisimu. Mifano ifuatayo inadhihirisha hili:

**Mfano wa kwanza**

Munyao: Wee Kasee wacha hizo. Hii kitu si *pend.*
Mueke: Sio mimi nasema, ni *system.*
Munyao: Kwani mbona mnasumbua Wakenya hivi? *You should be patriotic.*
Mueke: Wewe sin i Mkenya na tena *patriot,* saidia wao. Weka hapa *sign* ndio niamini.

**Mfano wa Pili**
Wamalwa: *Excuse me boss*, ile *case* ya Hajj tufanyeje?
Scolla: *Of course it has to go through the office. I hope* ame-*avail all the required documents.*
Wamalwa: Ndiyo *madam*, *but* hana barua ya *chief.*
Scolla: *You know very well requirements* za *Hajj applications*. Lazima applicant alete barua ya chief, barua ya *Council of Imams* au *Supkem*, *next of kin*, *ID copies and original ID & BC plus copies.*

**Mfano wa Tatu**
Afisa A: *Excuse me madam boss, I want to consult something.*
Afisa B: Kwani wewe huoni niko *busy*, unapenda kunisumbua sana.
Afisa A: Sorry, ni hivi, hii bc haina authority number na ni late registration.
Afisa B: Kwanza hata *BC* yenyewe haina *seal*.

**Mfano wa Nne**
Afisa C: Hallo, naulizaje unangalilie hii kama ***R*** *number* yake ni same na ya babake.

Afisa D: Wapi *passport number* yake.
Afisa C: Hana ndio sababu nataka *u track* kwa *system*. *Passport* ilipotea.
Afisa D: Nani anataka *passport*?

**Mfano wa Tano.**
Afisa E: Wee *boss,* uko wapi leo?
Afisa F: Niko *counter five*.

Ni dhahiri katika mazungumzo haya kwamba uchanganyaji msimbo na uhamishaji msimbo ni tukio la kawaida kabisa katika mawasiliano baina ya wanaidara. Kutokana na hali kwamba viwango vya elimu vinawawezesha kuwa na ufahamu na umilisi wa Kiswahili na Kiingereza, wanazitumia lugha hizi mbili kwa kubalidisha mara kwa mara. Kwa misingi ya jinsia, ilidhihirika kuwa wanawake waliorekodiwa katika utafiti huu walichanganya na kuhamisha msimbo zaidi kwa mazoea kuliko wenzao wa kiume.

## 3.3 Hitimisho

Ilivyobainika katika data hii, ni dhahiri kwamba uchanganyaji na uhamishaji msimbo ni jambo la kawaida palipo na mahusiano ya watumizi lugha zaidi ya moja. Wanaidara baina yao huchanganya na kuhamisha misimbo katika mikutadha na nafasi mbalimbali za utumizi lugha na vilevile wao hubadili na kuhamisha msimbo katika hali fulani za kuwasiliana na wahudumiwa wanapoendelea kuwahudumia. Wahudumiwa nao hudhihirisha uhamishaji na uchanganyaji msimbo katika hali mbalimbali za mawasiliano na wanaidara wanaowahudumia. Hata hivyo, katika Idara ya Uhamiaji mjini Mombasa ni dhahiri kwamba uchanganyaji msimbo ni katika misingi ya umri, jinsia na viwango vya elimu. Kutokana na viwango vya elimu na umahususi wa istilahi mbalimbali za kiidara, uhamishaji na uchanganyaji msimbo ni jambo linalotarajiwa hasa miongoni mwa wanaidara. Lugha katika Idara ya Uhamiaji hushamiri uchanganyaji na uhamishaji msimbo kutokana hali na mikutadha hii mbalimbali inayoelekeza utumizi lugha.

Kwa kuzingatia kigezo cha umri na lugha zinazopendelewa, majibu ya hojaji yalibaini kuwa asilimia kubwa sana ya vijana na hasa waliosoma hupendelea kutumia lugha ya kiingereza ikilinganishwa na wazungumzaji wa umri wa zaidi ya miaka hamsini. Hii ni kutokana na idadi watu kumi kati ya kumi na tano waliojaza hojaji kuwa na msimamo huo. Jambo lingine lililojitokeza ni kuwa lugha za asili hutumika sana katika mazingira ambapo wazungumzaji hawana ufahamu wa lugha nyingine au iwapo ufahamu huo upo basi ni kwa kiwango cha chini mno. Wazungumzaji kama hawa huchangamkia lugha zao asili wanapokutana na afisa anayeweza kuzungumza lugha hizo zao za asili. Hii ni tofauti na wenzao ambao ni wa kutoka jamiilugha moja na afisa anayemhudumia na ambao wameelimika. Wazungumzaji waliosoma hadi kiwango fulani hutaka kujihusisha na lugha ya Kiingereza au Kiswahili licha ya kujaribu kuzungumziwa kwa lugha zao asili.

Ugunduzi mwingine ni kuwa mseto wa lugha hutumika wakati wa mazungumzo yanayohusisha maafisa wa idara ya uhamiaji wanapowasiliana wao kwa wao. Mazungumzo kama haya huhusisha lugha za kiasili, lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili na mchanganyiko wa lugha mbili au zaidi wakati wa mawasiliano. Hata hivyo, lugha iliyopatikana kutumika kwa wingi wakati wa mawasiliano rasmi katika afisi za idara ya uhamiaji ni ya Kiingereza ikifuatiwa na Kiswahili. Ilidhihirika hata hivyo kwamba lugha ya Kiingereza ndio hutumika sana wakati maafisa wa cheo cha chini wanapozungumza na wale wacheo cha juu hasa wakati wa mawasiliano rasmi. Hali hii hubadilika wakati maafisa hawa wa idara ya uhamiaji wanapowasiliana na wazungumzaji mbalimbali wanaoleta maombi ya pasipoti katika afisi za idara ya uhamiaji. Mawasiliano wakati huu hubadilika kutegemea wazungumzaji mbalimbali ambao hutofautiana kwa misingi ya kiwango cha elimu, umilisi wa lugha husika, mila na tamaduni za wazungumzaji miongoni mwa mambo mengine.

# SURA YA NNE

# SENTENSI KATIKA LUGHA YA IDARA YA UHAMIAJI

## 4.0 Utangulizi

Sentensi zilizochunguzwa zilitokana na baadhi ya mazungumzo yaliyotokea katika idara ya uhamiaji. Sehemu hii inahusu uchanganuzi wa deta tuliyoikusanya kwa kubaini aina za sentensi zilizotumika katika suala zima la matumizi ya lugha katika idara ya uhamiaji nchini Kenya. Haya yalifanyika kwa misingi ya nadharia ya kundi ndani na kundi nje ya Giles (1979) pamoja na kuzingatia mawazo ya Bernstein (ashatajwa) juu ya msimbo finyu na msimbo pana. Wahusika tofauti walitumia aina mbalimbali za sentensi katika mazungumzo yao katika afisi za idara ya uhamiaji, Mombasa.

## 4.1 Sentensi za Kimuundo kwa Jumla

Mazungumzo ya wafanyikazi katika idara ya uhamiaji yalidhihirisha mseto wa sentensi. Kimuundo kuna aina tatu za sentensi – sahili, ambatani na changamano. Hizi ndizo aina tatu za sentensi ambazo zilijitokeza katika mazungumzo baina ya maafisa wa idara ya uhamiaji na waombaji pasipoti katika afisi za idara ya uhamiaji Mombasa. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ilidhihirika kuwa sentensi zilizoongoza kwa wingi wa matumizi ni sentensi sahili. Mazungumzo yaliyofanyika katika afisi za idara ya uhamiaji yalisheheni sentensi nyingi sahili kuliko aina nyingine ya sentensi. Inavyoelekea, wazungumzaji wengi walitumia sentensi sahili kwa kujibu maswali yaliyohitaji majibu ya moja kwa moja bila kutoa ufafanuzi zaidi. Wengi wa wazungumzaji waliotoa majibu yao kwa njia ya moja kwa moja walifanya hivyo kwa kutoa majibu mafupi yaliyojitokeza katika sentensi sahili.

Sentensi sahili zimetumika kwa sababu ya haja ya iktisadi ya maneno pamoja na chukulizi kwamba kile kinachosemwa kinaeleweka kimuktadha na kwa hivyo hakihitaji ufafanuzi zaidi. Hoja hii inaingiliana na mawazo ya Bernstein (1971) kuhusu msimbo finyu na msimbo pana. Hii ni kwa sababu wafanyikazi katika idara ya uhamiaji wanao uzoefu wa utendakazi wao na kwa

hivyo si lazima wanaoomba vyeti vya kusafiria watoe maelezo mengi kuhusu shughuli hii. Kati ya sentensi mia moja zilizochunguzwa, sentensi hamsini na tatu zilikuwa sahili. Hii ni asilimia hamsini na tatu ya jumla ya sentensi zilizochunguzwa. Idadi hii ni dhihirisho kuwa sentensi sahili zinatumika kwa wingi sana kuliko aina nyingine za sentensi katika idara ya uhamiaji.

Sentensi ambatani zilikuwa thelathini. Hii ni asilimia thelathini ya jumla ya sentensi zilizofanyiwa uchunguzi. Aina ya tatu ya sentensi zilizochunguzwa zilikuwa sentensi changamani. Jumla ya sentensi kumi na saba kati ya zile mia moja zilizochunguzwa zilikuwa sentensi changamani. Hii ni asilimia kumi na saba ya jumla ya sentensi zilizoshirikishwa katika utafiti huu. Matokeo haya yanaweza kuwasilishwa kwa mchoro wa pai chati kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Sentensi sahili – asilimia hamsini na tatu (53%)

Sentensi ambatani – asilimia thelathini (30%)

Sentensi changamani – asilimia kumi na saba (17%)

Kwa kuzingatia jinsia, ilibainika kuwa wanawake walitumia sentensi sahili kwa wingi ikilinganishwa na wanaume. Kati ya sentensi hamsini na tatu zilizotumika, thelatini na mbili zilitumiwa na wanawake huku ishirini namoja zikitumiwa na wanaume. Hii ni asilimia 60.37% kwa wanawake huku wanaume wakitumia sentensi sahili kwa asilimia 39.6%.

Matokeo haya yanaonekana kukinzana na maoni ya wanaisimu wengi kuwa lugha ya wanaume ndio kavu na kali isiyoonyesha hisia. Wanaume hukatizana na hawapishani katika mazungumzo jambo linaloleta kutoelewana na kutinga mawasiliano. Hawazingatii usikilizaji na wanatumia lugha ya kuamrisha. Mara nyingi hawatumii majina ya wahusika na huhifadhi mitindo ya kizamani na kitamaduni. Wanawake kwa upande wao hudhihirisha sifa kinyume na hizi za wanaume.

Hata hivyo, hali ilikuwa tofauti na sentensi ambatani na changamani ambapo wanaume walitumia sentensi hizi kwa wingi ikilinganishwa na wanawake. Kati ya sentensi thelathini ambatani zilizotumika katika utafiti huu, kumi na nane zilitumiwa na wanaume huku kumi na mbili zikitumiwa na wanawake. Hiyo ni asilimia sitini (60%) kwa upande wa wanaume na asilimia arobaini (40%) kwa upande wa wanawake. Hali hii pia ilijitokeza katika matumizi ya sentensi changamani ambapo wanaume walitumia sentensi tisa kati ya kumi na saba zilizotumika. Hii ni asilimia hamsini na mbili ya sentensi changamani zilizotumika. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo haya ya matumizi ya aina mbalimbali za sentensi kwa misingi ya jinsia.

**Jedwali 4: Aina za Sentensi kwa Misingi ya Jinsia.**

| Aina | Wanaume | Wanawake | | Jumla | % Wanaume | %Wanawake |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Sahili | 21 | 32 | | 53 | 39.6 | 60.4 |
| Ambatani | 18 | 12 | | 30 | 60 | 40 |
| Changamani | 9 | 8 | | 17 | 52.9 | 47.1 |
| Jumla | 48 | 52 | | 100 | 48 | 52 |

Kama inavyojitokeza katika jedwali hili, wanawake walielekea kuzipendelea zaidi sentensi sahili kuliko wanaume ambao nao walipendelea sentensi ambatani na changamani. Inawezekana kuwa matumizi ya sentensi sahili kwa wingi inatokana na chukulizi kwamba kile kinachosemwa kinaeleweka kimuktadha na kwa hiyo hakihitaji ufafanuzi zaidi.

## 4.2 Sentensi katika Lugha baina ya Wanaidara na Wahudumiwa

### 4.2.1 Sentensi Sahili

Sentensi sahili ndizo zilizotumika kwa wingi na wahudumiwa. Sentensi sahili kama zilivyotumika na wafanyikazi zilichukua miundo au maumbo mbalimbali. Kulikuwa na sentensi sahili za neno moja na sentensi sahili zilizokuwa na kundi nomino na kundi tenzi. Zifuatazo ni sentensi sahili za neno moja kama zilivyotumiwa na wafanyikazi.

1. Utaleta?
2. Hatutakubali.
3. Utamleta.

Sentensi hizi zinadhihirisha muundo wa neno moja. Hata hivyo, hizi ni sentensi zilizokamilika kabisa kama inavyoonekana kupitia uchanganuzi wake ambao unadhihirisha sehemu zote za sentensi.

Utaleta- U---ta---let---a

Hatutakubali – HA---tu---ta---kubal---i

Mbali na sentensi sahili za neno moja, kulikuwa na sentensi sahili zilizokuwa na KT na KN. Mifano ifuatayo ilijitokeza katika matumizi wakati wa mazungumzo ya wafanyikazi.

1. Shule unasoma wapi?
2. Mama anaitwa nani?
3. Nyumbani ni wapi?
4. Code yake ni gani?
5. Place of birth ndio shida yangu
6. Hospitali hiyo iko wapi?
7. Hii birth certificate uliichukua wapi?
8. Yeye mwenyewe hatumhitaji.

9. Mama yako ndiye aliyekupatia?

10. Picha zako ziko wapi?

11. Kitambulisho chako?

12. Shule ulisomea wapi?

13. K.C.S.E ulifanya lini?

14. Soma hili jina.

15. Anaishi Mtwapa.

16. Mke wako ulimwoa lini?

16. Urafiki huo wenu uliisha mwaka gani?

17. Funyula imekuwa kubwa sana siku hizi.

18. Lawyer atamwandikia affidavit.

19. Wewe hujui Kiswahili?

20. Baba alikuwa akifanya kazi gani?

21. Mke wako wa kwanza alikuwa akiitwa nani?

Sentensi hizi kwa wingi zilijitokeza kama maswali yaliyoulizwa wale wahudumiwa waliofika katika afisi za Idara ya Uhamiaji kwa nia ya kuomba pasipoti. Ni maswali yaliyoulizwa na maafisa wa Idara ya Uhamiaji katika jitihada zao za kuminya habari muhimu kuhusu wahudumiwa hawa. Wahudumiwa nao walidhihirisha matumizi haya ya sentensi sahili na fupi. Hizi zilijitokeza sana katika majibu yao kwa maswali waliyokuwa wameulizwa na wanaidara. Zifuatazo ni baadhi ya sentensi hizo kama zilivyojitokeza katika mazungumzo ya wahudumiwa hawa:

1. Mama alifariki mwaka jana.
2. Nimeleta

3. Tutasafiri
4. Baba alipotea
5. Anaishi Mtongwe mama
6. Baba hana birth certificate
7. Nilipata ID kitambo sana
8. Aliyenipatia hii birth ni mama
9. Huyo ni ami yangu
10. Mimi naitwa Benard
11. Picha zangu ziko hapa ndani
12. Hiki hapa kitambulisho chake
13. Mumewe ndiye anayeishi Ughaibuni
14. Chifu wetu anaishi Kibokoni
15. Mama anafaa asafiri Jumapili hii
16. Mzee yule mkongwe ametoka Ukunda

### 4.2.2 Sentensi Ambatani

Sentensi ambatani ni zile sentensi ambazo zina muundo wa vishazi huru viwili au zaidi, vilivyounganishwa kwa viunganishi ambatani. Viunganishi hivi ni kama; na, lakini, ilhali, miongoni mwa viunganishi vingine. Viunganishi hivi huja baina ya vishazi hivi vilivyoambatanishwa na hivyo haviwezi kuja mwanzoni mwa sentensi. Sentensi nyingi ambatani zilijitokeza katika utafiti huu uliofanyika katika afisi za idara ya uhamiaji Mombasa. Ni sentensi zilizotumiwa na wafanyi kazi wa pale idarani pamija na wahudumiwa waliofika katika afisi hizo kwa minajili ya kuja kuomba pasipoti. Zifuatazo ni baadhi ya sentensi hizo kama zilivyotumika katika afisi za idara ya uhamiaji:

1. Hapa lazima ibadilishwe ***la sivyo*** application yako itakataliwa.

2. Kwa birth certificate wameandika umezaliwa Kisauni ***ilhali*** kitambulisho chako wameandika Msambweni.
3. Hii birth utaenda kurekebisha ***kwa*** sababu iko faulty.
4. Utaenda pale nje utoe copy ya hizi mbili ***kwa sababu*** tutakurudishia originals zako.
5. Mahali pa kuchukulia kitambulisho panaweza kubadilika ***kwa sababu*** mtu anaweza kuchukua kitambulisho akiwa mahali popote nchini.
6. The original birth certificate is here ***but*** what Iam asking for is a copy of the certificate.
7. Point noted Samira, ***but*** we don't encourage business in this area.
8. Wanawake na watoto watahudumiwa hapa ***lakini*** wanaume wote wataenda pale.

Kama ilivyotajwa hapo awali, wahudumiwa mbalimbali waliofika katika afisi za Idara ya Uhamiaji kuleta maombi ya pasipoti walitumia sentensi ambatani jinsi tu walivyofanya wafanyikazi. Zifuatazo ni baadhi ya sentensi ambatani kama zilivyojitokeza katika mazungumzo ya wahudumiwa waliofika katika afisi za uhamiaji kuleta maombi ya pasipoti.

1. Sister yangu ndiye aliyenipa hii birth ***lakini*** alipewa na mama yetu.
2. Mimi nimezaliwa Ma Fatma hospital ***ila*** nimelelewa Msambweni.
3. We have come to apply for passports ***becuse*** we are supposed to travel soon.
4. Mama alipoteza ID yake ***but*** I have brought her waiting card.
5. Mimi naitwa Samira ***and*** my sister here is called Shamsa.
6. Mama alipoteza *ID* yake ***but*** nilikuwa nimeshafanya copy zamani ***ndiyo sababu*** nimekuja nayo.
7. Mimi naitwa Shaneez ***na*** huyu hapa auntie yangu Zamzam.
8. Our father is a car dealer ***but*** mum is just a housewife.

9. My father said the papers are in order ***and*** therefore we don't expect any problem with our documents.
10. My brother is Hamisi ***and*** he goes to school at Fadhili Academy.

### 4.2.3 Sentensi changamani

Utafiti huu ulibaini matumizi ya sentensi changamani katika mazungumzo yaliyotokea katika afisi za idara ya uhamiaji. Kulikuwa na sentensi changamano za kishazi tegemezi cha masharti na pia kulikuwa na sentensi changamani za kishazi kitegemezi rejeshi. Matumizi ya sentensi changamani hata hivyo hayakuwa ya kiwango cha juu kama ilivyokuwa na matumizi ya sentensi sahili na sentensi ambatani. Zifuatazo ni sentensi changamani zilizotumika katika utafiti huu kama zilivyojitokeza katika mazungumzo ya wafanyikazi na wageni katika afisi za idara ya uhamiaji Mombasa.

1. Usipoleta original birth certificate, application yako haitachukuliwa.
2. Usiporekebisha hii birth kwanza, hautaweza kupata passport.
3. Utaleta waiting card ukitaka passport yako itengenezwe.
4. Utamleta mama yako ndipo tuamini unayoyasema.
5. Watu wanaotaka ku apply passport wanapeana forms zao pale nje kwanza zikaguliwe.
6. Ukileta affidavit tuta process passport yako.
7. Pasipoti ambayo niliichukua jana wamekosea kuandika jina langu.
8. Copy ambayo ulinituma nilete nimempa yule afisa.
9. Stakabadhi nilizoitishwa juzi nimezileta leo.

Sentensi hizi hudhihirika zaidi wakati kunapohitajika maelezo marefu kuhusu jambo au kitu. Kutokana na mifano ya sentensi zinazodhirika hapa, hata pale sentensi hizo zilipotumiwa kujibu swali la mwanaidara au afisa wa idara ya uhamiaji, sentensi hiyo ilitumiwa aghalabu katika

kutoa maelezo. Baadhi zilidhihirika katika uchanganyaji na uhamishaji msimbo lakini ikabaki ile ile ya sentensi changamani ya kufafanua au kutoa maelezo ya kina kuhusu suala.

**4.3 Sentensi za lugha baina ya wanaidara**

Zifuatazo ni baadhi ya sentensi zilizojitokeza katika mazungumzo yaliyohusisha wanaidara wakati wa shughuli zao mbalimbali katika maeneo yao ya kazi katika afisi za Idara ya Uhamiaji.Sentensi hizi zimeorodheshwa bila ya kuzitenganisha katika aina mbalimbali ya sentensi.

1. Wewe huoni niko busy.
2. Hii bc haina authority and yet ni late registration. (ambatani)
3. Wazazi wake wanatoka wapi?
4. Wapi passport number yake?
5. Wewe unapenda kunisumbua sana.
6. Mimi niko counter five.
7. Kwani umetoka verification?
8. Nimeambiwa nishikie Savini coz yuko vetting.
9. Ni mtoto mdogo ndio sababu twatumia file ya babake.
10. Wacha niendelee na kazi yangu.
11. Hakuna ndio nataka uingalie kwa system.
12. Please confirm kama hiyo application iko sawa.
13. Kwanza hiyo format ametumia ni mbaya.
14. Si huyu ni mtu wenu, wewe ongea naye.
15. Ukitrack inasema shida iko wapi?
16. *You know very well requirements* za *Hajj applications*. Lazima applicant alete barua ya

chief, barua ya *Council of Imams* au *Supkem*, *next of kin*, *ID copies and original ID & BC plus copies.*

Kwa misingi ya jinsia, ilidhihirika kuwa wanawake waliorekodiwa katika utafiti huu ambao ni maafisa wa idara ya uhamiaji walitumia sentensi ambatani kwa wingi ikilinganishwa na wanaume ambao walionekana kutumia sentensi sahili kwa wingi zaidi. Hata hivyo wahusika wote katika kundi hili walitumia sentensi sahili kwa wingi kuliko aina nyingine yoyote ile ya sentensi. Sentensi changamani ndizo zilizotumika kwa uchache zaidi. Wingi wa sentensi hizi zilijitokeza kama maswali yaliyowalenga wahusika waliofika kwa minajili ya kuleta maombi ya pasipoti. Sentensi zenyewe zilizingatia miundo mbalimbali ya mpangilio wa maneno.

Jambo lingine lililozingatiwa wakati wa kuchunguza sentensi zilivyotumika katika utafiti huu ni tajriba na uzoefu wa kazi. Kama ilivyoelekea, maafisa walio na uzoefu wa miaka mingi katika kazi yao walionekana wepesi wa kubadili na kuchanganya aina mbalimbali za sentensi ikilinganishwa na wenzao ambao hawana uzoefu wa miaka mingi. Hivyo, wingi wa sentensi ambatano na changamani zilizotumika zilitumiwa na maafisa ambao wamefanya kazi idarani kwa miaka mitatu hivi au zaidi.

Matumizi ya sentensi kwa misingi ya kiwango cha elimu hayakuonyesha tofauti yoyote ikizingatiwa kuwa wahusika wote wana elimu ya kiwango cha chuo kikuu. Inavyoelekea, kiwango hiki cha juu cha elimu walicho nacho maafisa wa idara ya uhsmiaji kilichangia pakubwa katika uwezo wa wahusika kutumia aina mbalimbali za sentensi na kwa kuzingatia miundo tofauti katika utunzi wa sentensi hizi.

### 4.4 Sehemu za sentensi zilizotumiwa badala ya sentensi nzima

Sentensi huwa na sehemu au vijesehemu mbalimbali ambavyo vina uamilifu wa kisarufi. Miongoni mwa sehemu hizi ni kiima, kiarifu, kundi nomino, kundi tenzi, shamirisho au yambwa, kirai, kishazi na chagizo miongoni mwa nyingine. Katika utafiti wetu tumejikita katika virai na vishazi kutokana na utukiaji wavyo wa mara kwa mara katika utumizi lugha wa idara ya

uhamiaji. Aidha, hata katika utukiaji huu si aina zote za virai wala aina zote za vishazi ambazo hudhihirika kutokea katika mawasiliano au lugha baina ya wanaidara. Lugha ya Kiswahili ambayo ni mojawapo ya lugha za kibantu huwa na muundo na mpangilio wa maneno ambao si rahisi kutabirika, japo kuna ule mpangilio wa kawaida na uliozoeleka wa kiima (S) + kitenzi (V) + yambwa (O). Watumizi lugha hata hivyo wanaweza kuamua kutumia sentensi kamilifu kuwasilisha ujumbe au kwa iktisadi ya maneno wakatumia sehemu ya sentensi kuwasilisha ujumbe wao. Iktisadi hii ya maneno ambayo ni moja katika mihimili ya nadharia ya Bernstein ya msimbo pana na msimbo finyu, huwawezesha watumizi kuwasiliana haraka bila kupoteza wakati au kuwasilisha ujumbe kwa haraka ndipo waweze kuwahudumia watu wengi.

Lugha katika idara ya uhamiaji inadhihirisha iktisadi hii ya maneno inavyosemwa katika nadharia ya iktisadi ya maneno. Watumizi lugha hufupisha au kubana lugha kwa kutumia maneno machache tu ambayo yanajitokeza kama sehemu mbalimbali za sentensi. Wanaidara wanaweza kutumia virai nomino pekee aghalabu katika maswali bila haja ya kutunga sentensi kamili. Na kwa kuwa sehemu hizi za sentensi zinaweza kueleweka katika mikutadha ya utumizi lugha hiyo, wahudumiwa ama wanaidara wanaoelekezewa kauli hizi huelewa na kujibu.

### 4.4.1 Virai

Kirai ni kipashio cha kisarufi ambacho kina zaidi ya neno moja lakini hakina uhusiano wa kiima-kiarifu, yaani hakihusishi mtendaji wa tendo na tendo linalotendwa. Ni kundi la maneno ambayo hayana ukamilifu wa maana. Kwa kuzingatia kichwa au neno kuu katika kirai, aina zifuatazo za virai ziliainishwa katika matumizi ya lugha katika Idara ya Uhamiaji.

#### 4.4.1.1 Kirai nomino

Kinaitwa kirai- nomino kwa sababu muundo wake umekitwa kwenye neno kuu (kichwa) ambalo ni nomino au kiwakilishi. Nomino yaweza kuwa wazi au ikawa imewakilishwa na kiwakilishi.

Katika kirai-nomino, mpangilio wake wa kawaida huwa na nomino ambayo ndiyo inayotangulia na kasha kufuatwa na kivumishi au vivumishi vinavyoangazia sifa za nomino hii. Kwa mfano;

*Kalamu hii nyekundu*

Lakini kuna kighairi kuwa kuna uwezekano wa vivumishi vionyeshi au viashiria kutokea kabla ya nomino. Inapotokea hivi, inakuwa kwamba kinachosisitizwa ni kionyeshi kuwa ni kalamu hiyo nyekundu na wala si nyingine yoyote. Ifuatayo ni mipangilio tofauti kama ilivyotokea katika mazungumzo yaliyofanyika katika afisi za idara ya uhamiaji.

1. Kitambulisho chako?
2. Hii hapa birth certificate.
3. Hospitali hiyo
4. Picha zako?
5. *Code* yake
6. Huyo ami

9. Chifu wetu mkali
10. Huyo msichana mweupe mrefu
11. Mke wako
12. Rangi ya macho yako?
13. Rangi ya macho ya dada yako?

Inavyodhihirika katika data hii, virai nomino vilitumiwa kuwasilisha majibu au kuuliza maswali baina ya wanaidara na wahudumiwa. Utumizi wa sehemu hizi za sentensi kuwasiliana badala asntensi kamili ni sehemu ya iktisadi ya maneno.

#### 4.4.1.2 Kirai kielezi

Kirai hiki ni tofauti na virai vingine kwa sababu katika muundo wake, si lazima uwe kwenye uhusiano na neon kuu. Vielezi hufafanua jinsi, wakati, mahali, na kinachofanya tendo lifanyike. Virai vielezi vinaweza kutokea mahali popote katika kishazi kwa sababu kinyume na kiima, kitenzi na yambwa, vielezi huwa havina uelekezi wowote. Katika lugha ya idara ya uhamiaji hata hivyo, virai vielezi vinaweza kujitokeza pekee au kwa kujisimamia bila kufungamana na sehemu nyingine za sentensi. Aghalabu hili ni dhahiri katika majibu yanayotolewa na wahudumiwa wanapoulizwa maswali yanayohitaji majibu ya kivielezi. Kwa mfano:

Mwanaidara: Ulimaliza *form four* lini?

Mhudumiwa: *Last year* (mwaka jana).

Hali hii ya kutumia vielezi vya wakati *mwaka jana* pekee katika kujibu swali la mwanaidara badala ya kutunga sentensi kamili yenye jumla ya kiima na kiarifu, ni mmoja katika mfano wa iktisadi ya maneno inayorejelewa katika nadharia ya iktisadi ya maneno. Ni jambo la kawaida kutumia sehemu hizi za sentensi au maneno katika mawasiliano kwenye idara ya uhamiaji kama nyenzo kudhihirisha iktisadi ya maneno.

### 4.4.2. Vishazi

Kishazi ni tungo ya kisarufi yenye mpangilio wa kiima na kiarifu kimoja ambayo inaweza kujisimamia kimaana au ikahitaji kukamilishwa kimaana kwa kufungamanishwa na kishazi kingine. Kwa maana hii kuna vishazi huru na vishazi tegemezi. Vishazi huru ni vile vilivyojikamilisha kimaana ilhali vishazi tegemezi vile visivyowasilisha maana kamili. Vishazi huru na tegemezi hutumiwa mara katika kujibu na kuuliza maswali katika lugha baina ya wanaidara na wahudumiwa katika idara ya uhamiaji. Kwa kuzingatia mifano mbalimbali kama ilivyotokea katika idara ya uhamiaji, vishazi hivi vilijitokeza.

1. *Lawyer atamwandikia affidavit.*
2. *Baba alimtaliki mama zamani.*

Ni muhimu kuzingatia kuwa vielezi vina uhuru mkubwa wa kutokea mahali popote katika vishazi kwa sababu kinyume na kiima, kitenzi na yambwa, vielezi huwa havina uelekezi wowote. Hili linadhihirika katika mifano hii hapa chini ambapo kielezi cha wakati kinaweza kutumika katika nafasi nne tofauti katika kishazi kimoja bila ya kuathiri maana.

Nilipata ID *kitambo sana.*

*Kitambo sana* nilipata ID.

ID *kitambo sana* nilipata.

Nilipata *kitambo sana* ID.

Inavyodhihirika katika mifano hii ya vishazi tuliyoitoa, maumbo na mpangilio wa maneno katika vishazi vyenyewe vinaweza kubadilikabadilika. Hili linaashiria kwamba sentensi zinavyotumiwa katika idara ya uhamiaji hazifungwi na kanuni za kisarufi zinazotarajiwa kwa kawaida katika sentensi ya Kiswahili. Hata hivyo, kwa kuwa lengo kuu huwa ni kuwasilisha ujumbe, vishazi hivi hutumiwa katika maumbo yoyote yale.

Aidha, utumizi wa akronimu za maneno badala ya maneno kamili ni mfano mwingine iktisadi hii ya maneno inayosaidia kufanikisha mawasiliano katika idara ya uhamiaji. Kwa mfano, mwanaidara anapotumia 'R number' badala ya 'reference number', 'BC' badala ya 'Birth certificate', KCPE na KCSE badala ya Kenya Certificate of Primary Education na Kenya Certificate of Secondary Education mtawalia, inadhihirika haja ya kufupisha na kuharakisha mawasiliano badala ya kutumia maneno mengi. Isitoshe, akronimu inaweza kueleweka rahisi ikiwa ndiyo inayotumiwa mara kwa mara katika mazoea ya utumizi lugha wa wahusika katika tukio hilo la mawasiliano.

## 4.5 Hitimisho

Ilivyodhihirika katika sura hii ama sentensi kamili au sehemu za sentensi hutumiwa kwa mawasiliano baina ya wanaidara na wanaidara na wahudumiwa. Haja ya kurahisisha na kuharakisha mawasiliano huwaishia wahusika katika utumizi lugha huu kupendelea sentensi sahili kimuundo badala ya aina nyingine za sentensi kimuundo na vipande au vijisehemu vya sentensi badala ya sentensi nzima kuwasiliana. Mifano ya data tuliyowasilisha katika sura hii inatoa ushahidi wa aina hii ya utumizi lugha na kuelekeza kuhusu sababu za kuteua kuitumia lugha katika mitindo hii mahsusi.

Viwango vya elimu na jinsia za watumizi lugha vimedhihirika kuwa na michango na ushawishi wa aina fulani katika sentensi zinazopendelewa na kuteuliwa na watumizi lugha hawa. Kwa maana hii, watumizi lugha wa jinsia ya kike kwa mfano wamedhihirika kutumia sentensi sahili kwa wingi kuliko wenzao wa kiume. Hili linaweza kushawishi au kuchochea kuendelea kwa mjadala unaofanyika kitaaluma kuhusu uwepo wa lugha za kijinsia na tofauti zake.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, CHANGAMOTO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Katika utafiti huu tulikusudia kuchunguza sifa za sajili ya idara ya uhamiaji kwa kurejlea vipengele viwili vikuu vya ubadilishaji msimbo na sentensi Katika sura hii hivyo basi tunaangazia muhtasari wa sehemu mbalimbali za tasnifu hii.

## 5.1 Muhtasari

Katika sura ya kwanza, tunatambua maazimio ya kazi hii kwa kujikita kuzingatia vipengele tangulizi vya pendekezo la utafiti. Hivi ni pamoja na kutambua usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete husika, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusiana na mada hii, mihimili ya nadharia mbili husika, pamoja na mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

Sura ya pili inachunguza kwa kina dhana na vipengele maalumu vya lugha ambavyo hutumiwa kama mihimili ya kubainishia sifa za sajili fulani ya lugha. Vipengele hivi amilifu kama vile sentensi, msamiati, ubadilishaji msimbo, kimbo na lugha ya kitamathali miongoni mwa vingine vinashughulikiwa kwa kina na kwa kurejelea baadhi ya mifano ya utukiaji wavyo katika muktadha wa idara ya uhamiaji.

Sura ya tatu inashughulikia uchanganuzi wa data inayohusu uchanganyaji na uhamishaji msimbo katika idara ya uhamiaji jijini Mombasa. Kwa kuwa mazingira ya utendakazi ya idara ya uhamiaji yanahusisha uhusika wa wanaidara wenyewe na kisha mazungumzo baina yao na wahudumiwa, tumechunguza uhamishaji na uchanganyaji kwa matapo haya mawili. Tumedondoa mifano ya utukiaji wa uhamishaji na uchanganyaji msimbo na kueleza sababu mbalimbali zinazochangia hali hizo katika mikutadha hiyo ya utumizi lugha.

Sura ya nne inachanganua kipengele cha kisintaksia na jinsi kinavyojitokeza katika utumizi lugha katika idara ya uhamiaji. Aina za sentensi kimuundo pamoja na sehemu za za kimuundo za sentensi ni miongoni mwa uamilifu tunaochunguza katika mazungumzo baina ya wanaidara na wahudumiwa na kisha wanaidara na wanaidara wenzao. Tunachunguza matumizi haya ya vijisehemu vya sentensi badala ya sentensi kamili kama kipengele cha iktisadi ya maneno ambacho ni muhimu ikizingatiwa utukiaji wake wa mara kwa mara.

Sura ya tano inawasilisha hitimisho jumuishi kutokana na uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Aidha, sura hii inaangazia changamoto zilizoukabili utafiti wetu, matokeo muhimu ya uchunguzi na mapendekezo kwa tafiti za baadaye.

Ili kuafikia malengo ya uchunguzi wetu, utukiaji wa ubadilishaji msimbo na miundo ya sentensi zinazotumiwa katika idara ya uhamiaji, utafiti wetu uliongozwa na nadharia tete mbili ambazo zilikuwa:

(i) Kuna viwango vya juu vya uhamishaji msimbo katika lugha inayotumiwa katika idara ya uhamiaji nchini Kenya.

(ii) Sentensi zenye miundo na maumbo mbalimbali yanayokiuka kanuni za kisarufi hudhihirika katika lugha ya idara ya uhamiaji nchini Kenya.

Tuliazimia kuchunguza vipengele mbalimbali vya nadharia ya ushirikishi na jinsi inavyochangia katika mazoea ya ubadilishaji msimbo katika mazungumzo baina ya wanaidara wenyewe kwa wenyewe na yale ya baina ya wanaidara na wahudumiwa. Aidha, kwa kuwa sentensi ni kipengele cha sintaksia tuliazimia kuangazia iktisadi ya maneno kama kipengele cha nadharia ya msimbo pana na msimbo finyu ikizingatiwa inavyojitokeza kwa wingi katika mazungumzo kwenye muktada huu.

## 5.2 Muhtasari wa matokeo

Kutokana na nadharia tete tulizokuwa tukitathmini, tuliafikia hitimisho kwamba lugha katika idara ya uhamiaji hushamiri ubadilishaji msimbo. Aidha, ilibainika kwamba iktisadi ya maneno hushawishi utumizi wa sehemu za sentensi badala ya sentensi kamili katika mawasiliano haya yanayohusisha ama wanaidara wenyewe kwa wenyewe au wanaidara na wahudumiwa.

### 5.2.1 Ubadilishaji msimbo

Uhamishaji na uchanganyaji msimbo ni jambo kawaida katika mawasiliano baina ya wanaidara na yale ya wanaidara na baadhi ya wahudumiwa. Utafiti huu ulibaini kuwa katika idara ya uhamiaji nchini Kenya kwa kutumia mfano wa utumizi lugha katika Idara ya Uhamiaji jijini Mombasa, ilibainika kwamba uhamishaji na ubadilishaji msimbo unahusisha kwa kiwango kikubwa lugha za Kiswahili na Kiingereza. Aidha, ilibainika kwamba hali hii ilikuwa bayana sana katika wahudumiwa waliopata elimu ya shule ya upili kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na wale ambao hawakufikia kiwango hicho cha elimu. Isitoshe, ilibainika kuwa lugha baina ya wanaidara wenyewe nayo ilishamiri uhamishaji na uchanganyaji msimbo kutokana na ukweli kwamba asilimia kubwa ya wafanyakazi hawa huajiriwa wakiwa tayari na elimu ya shule za upili au baada ya shule za upili kama vile vyuo vikuu.

Uhamishaji na uchanganyaji msimbo ulidhihirika sana katika kiwango cha leksimu au msamiati na wakati mwingine katika kurejelea istilahi ambazo tafsiri zake ama hazimo katika lugha ya mazoea ya watumizi lugha hawa au ni vifaa ambavyo vimezoeleka zaidi katika lugha pokezi ya uhamishaji huo. Kwa hivyo, watumizi lugha hawa walifanya mazoea kuhamisha na kuchanganya msimbo kila walipokosa istilahi au msamiati wa kutumia au walipokuwa katika haraka ya mawasiliano na hivyo hapakuwa na muda wa kuchuja au kutafuta msamiati na istilahi mwafaka kwa neno au maneno hayo waliyohamisha.

### 5.2.2 Sentensi

Kando na hali ya kawaida iliyobainika ya ubadilishaji msimbo, sentensi na sehemu za sentensi zilijitokeza kutumiwa katika upekee fulani. Kwanza, ilidhihirika kwamba matumizi ya sentensi sahili ni ya mara kwa mara katika makundi yote mawili yanayohusika katika utumizi lugha katika idara ya uhamiaji. Yamkini, sentensi sahili zilijitokeza kutumiwa kwa wingi sana kuliko aina nyingine za sentensi kimuundo. Hili tulilieleza kimsingi kama zao la kutotaka kupoteza wakati katika mawasiliano wala kutumia lugha ya kimzunguko. Isitoshe, sehemu za kimuundo za sentensi kama vile virai na vishazi vilionekana kutumika kutokana katika mahusiano ya kimawasiliano baina ya wahusika hawa. Utumizi huu wa sentensi sahili kwa wingi na uwezekano wa kutumika kwa vipande tu vya sentensi kulituishia kutazama iktisadi ya maneno kama nyenzo muhimu ya kuokoa muda katika mawasiliano baina ya wahusika hawa.

Idara ya Uhamiaji inawashughulikia watu wengi na inahusu masuala nyeti yakiwemo ya kiusalama. Kutokana na hali hii, haja ya kuharakisha shughuli na kuzingatia umakinifu kazini ni mambo ya kimsingi ambayo kivyovyote vile hayawezi kumpa mhudumiwa au mfanyakazi wa idara kutumia muda mwingi kueleza habari anazozitaka. Kwa maana hii, iktisadi ya maneno kama mtindo mwingine wa mawasiliano na utumizi lugha kulingana na iktisadi ya maneno, itajitokeza kama moja katika sifa kuu za kutambulisha sajili ya lugha katika idara ya uhamiaji.

## 5.3 Changamoto zilizoukabili utafiti huu

Utafiti huu ulikumbana na changamoto kadhaa. Kwanza haikuwa rahisi kukusanya data kutoka kwa watu waliokuja afisini kwa ajili ya kuwasilisha maombi ya pasipoti kwani walionekana tu kushughulikia suala hilo lililowaleta. Pia, maafisa wa idara ya uhamiaji mwanzoni hawakutaka kurekodiwa kwa kushuku iwapo mazungumzo hayo yangetumika kwa shughuli nyingine yoyote kando na utafiti huu. Changamoto nyingine ya utafiti huu ni kuwa afisi za idara ya uhamiaji zina shughuli nyingi sana na watu wengi jambo linalofanya mahali hapo kuwa na kelele na zogo

nyingi. Hii ni changamoto kwa kuwa mara kwa mara mazungumzo yaliyonuiwa kurekodiwa yalikumbwa na hitililafu kutokana na mwingiliano wa sauti nyingine pale idarani ambazo hazikunuiwa. Changamoto ya tatu ni kuwa utafiti huu uligharimu fedha nyingi hasa ikizingatiwa kuwa kulihitajika vifaa kwa kurekodi mazungumzo haya na vifaa hivi ni vya gharama ya juu.

**5.3 Hitimisho**

Utafiti huu ulinuia kubainisha aina za sentensi na miundo ya sentensi ambazo hupendelewa katika mazungumzo yanayofanyika katika afisi za idara ya uhamiaji. Aidha, utafiti huu ulijishughulisha na kubaini viwango vya ubadilishaji msimbo na sababu za kufanya hivyo katika matumizi ya lugha katika idara za uhamiaji nchini Kenya. Hili lilifanyika kwa kuangazia mazungumzo katika afisi za idara ya uhamiaji jijini Mombasa. Maswali ya utafiti yaliyoongoza uchunguzi huu yalitokana na makadirio tuliyokuwa nayo kutokana na mawazo yanayoibuliwa na nadharia tulizozitumia; ya Ujumlishaji wa kiusemi na ya msimbo pana na msimbo finyu ya Bernstein. Katika ujumlishaji wa kiusemi (accomodation), inadhihirika katika utafiti huu kwamba ubadilishaji msimbo ni zao la kutotaka kuwapoteza wengine katika tukio lolote la mawasiliano baina ya wahusika katika idara hii. Yaani, pale ambapo mzungumzaji hataki kumpoteza wala kumtaabisha mwenziwe kutafuta istilahi au msamiati fulani katika lugha chanzi analitumia neno la mazoea katika lugha pokezi na hili linadumisha ushirikiano baina yao hivyo basi kufanikisha mawasiliano hata zaidi. Uchanganyaji msimbo huu sawa na aina za sentensi vilionekana kutofautiana kutokana na tofauti za kijinsia na kielimu. Kwa maana hii, viwango vya elimu na tofauti za kijinsi vilijitokeza kama nguzo muhimu zinazoweza kutumiwa kupimia amali hizi za utafiti wetu.

Utafiti huu ulibainisha kuwa wazungumzaji wengi katika idara ya uhamiaji hutumia sentensi sahili na miundo ya sentensi isiyo sentensi kamili wanapowasiliana pale afisini. Hii ni sehemu ya iktisadi ya maneno ambayo kutokea kwake kulichunguzwa na kazi hii. Kuna uwezekano pia

kuwa sababu kuu ya matumizi ya sentensi sahili kwa wingi kuliko ambatani na changamani ni kutokana na chukulizi kuwa wazungumzaji walielewa kilichokuwa kikizungumziwa na hivyo hakukuwa na haja ya ufafanuzi zaidi.

### 5.4 Mapendekezo kwa utafiti wa baadaye

Kwa kuwa utafiti huu ulibanwa kwa upeo na mipaka, ni sehemu ndogo tu ya uchunguzi wa matumizi ya lugha katika idara ya uhamiaji iliyoshughulikiwa. Kwanza ni kuwa utafiti huu uliangazia matumizi ya lugha katika kitengo kimoja tu cha idara ya uhamiaji ambacho ni kitengo cha pasipoti. Ukweli ni kwamba idara ya uhamiaji ina vitengo vingi ambavyo watafiti wa baadaye wanaweza kushughulikia. Aidha, katika kitengo hiki cha utoaji wa pasipoti kuna wafanyakazi wanaofanya kazi mbalimbali wakiwemo wanaoshughulikia usafi na maslahi ya kiafya ya wanaidara wengine. Lugha inayotumiwa na hawaikuchunguzwa kwa hivyo tafiti za baadaye zinaweza kuangazia hali hii. Isitoshe, katika uhamishaji, usanifu na urasmi katika matumizi ya lugha, utafiti huu ulielekea kubaini kwamba ngazi za kimamlaka au vyeo zilikuwa na mchango na athari mbalimbali katika utumizi lugha idarani humu. Tafiti za baadaye zinaweza kufungamanisha masuala haya ya utumizi lugha kama zao la athari ya tofauti za kimamlaka

## MAREJELEO


Bernstein, B. (1971) *Class, Codes and Control: Theoretical Studies Towards a Sociology of Language.* London: Routledge and Kegan Paul Publishers.

Binyanya, M. R. (2014) *Sajili ya Maafisa wa Polisi: Tathmini ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kituo cha polisi cha Central Nairobi.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Brown, S. (1999): *The Syntax of Negation in Russian: A Minimalist Approach.* Stanford: CSLI Publications

Crystall, D. (1997) *Dictionary of Linguistics and Phonetics*, 4th edition.

Giles, H. (1975) *Speech, Style and Social Evaluation.* London: Academic Press INC.

Gumperz, J.J. (1982) *Discourse Strategies.* Cambridge: Cambridge University Press.

Habwe, J (2010) *Darubini ya Isimujamii*: Nairobi: Focus Publishers.

Habwe, J (1999) *Discourse Analysis of Kiswahili Speeches.Tasnifu ya Uzamifu*, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Heredia, R.R. & Altariba, J. (2001*) Bilingual language mixing: why do bilinguals code-switch?* Toleo 10 (5)

Iribemwangi, P.I. na Mukhwana, A. (2010) *Isimujamii.* Nairobi: Focus.

Kimaiyo, P (2014) *The Markedness Model Approach to the Motivation and Functions of Code-Switching and Code-Mixing: A case study of selected Kipsigis songs.* Tasnifu ya uzamili, chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mathooko, P.M. (2007) *Isimujamii: Misingi na Nadharia.* Nairobi: Njigua Books.

Mekacha, D.K. (2011) *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili.* Dar-es Salaam: Osaka University of Foreign Studies.

Michira, J.N. (1993) *Uchanganuzi wa kimtindo wa lugha ya wachuuzi na lugha ya matangazo ya*

*biashara redioni.* Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Myslin, M. & Levy, R. (2015) '*Code-switching and Predictability of meaning in Discourse*' Katika: *Language*. Toleo 91 (4)

Njenga, P. (2008) *English-Kiswahili Code-switching in Easy F.M: The Markedness Model.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Nyaga, R (2013) *Code-switching in Political Speeches: A case study of selected Presidential Campaign Speeches in Kenya.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Obuchi, S.M. (2008) *Discourse Structure of Trader-Customer Kiswahili Interactions in Kenya Open-Air Markets: A Case of Gikomba and Kongowea.* (Tasnifu ya Uzamifu ambayo Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi

Rose, S (2006) *The Functions of Code-switching in a Multicultural High School. Mphil. Thesis in Intercultural Communication*: Stellenbosch University.

Wanjugu, V. (2010) *Sababu na Athari za Ubadilishaji msimbo shuleni: Utafiti katika shule ya upili ya Akiba.*Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Wardhaugh, R (2010) *Introduction to Sociolinguistics*. Oxford: Blackwell.

Waweru, T (2014) *Matumizi ya lugha katika kanisa Katoliki: Uchanganuzi wa ubadilishaji msimbo katika mahubiri.* Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho cha Kwanza

Yafuatayo ni mazungumzo baina ya kijana wa umri wa miaka ishirini aliyeleta maombi ya pasipoti katika idara ya uhamiaji na afisa wa idara ya uhamiaji. ni kuwa. Amehitimu kidato cha nne na ananuia kujiunga na chuo kikuu nchini India.

Afisa: *Next, yees.* Karibu kiti.
Mwengo: (Akiketi) *Thank you sir.*
Afisa: Habari yako kijana, nikusaidie vipi?
Mwengo: Well, thanks. My name is Athman Mwengo and Ihave come to apply for a passport.
Afisa: You are welcome. Now can I have your filled application forms and other documents please?
Mwengo: (Akimpatia) Here. They are all there in this envelope including my passport size photos.
Afisa: (Akikagua fomu ya maombi ya pasipoti) this form is incomplete. Why haven't you filled all the parts of the form? Here for instance, what is your height? Do you know your height?
Mwengo: To be sincere Iam not sure.
Afisa: Haya, nenda pale uambie yule afisa akupime halafu urudi. (Akiashiria kwa kidole) Pale.
Mwengo: (Akiondoka) Sawa.
*Baada ya muda mfupi*
Afisa: Amekwambia ni ngapi.
Mwengo: Its 5' 4.
Afisa: Sawa. Na hapa pia hukujaza. Whats the colour of your eyes?
Mwengo: I don't know sir.
Afisa: You don't know the colour of your eyes? Ok, can I write green?
Mwengo: (Akicheka) No sir, Idon't think they are green.
Afisa: Then what colour are they? (Akimwangalia). It's black. We normally look at the pupil of the eye not the entire eye. It can either be black or brown. Yours is black. (Anaandika)
Mwengo: Thank you sir.
Afisa: Your address. Why didn't you fill this part?
Mwengo: My parents don't have an address. Maybe I use the one for my former school.
Afisa: Its okay, what is the address?
Mwengo: It is Box 133, Kilifi.
Afisa: (Akiandika) *Code* yake ni nini?
Mwengo: Idon't know that one.
Afisa: Reason for travel?
Mwengo: Academics. Studies. Iam one of the students who were selected by the county government to go and further our studies in India. We are a group of fourteen students.
Afisa: Congratulations.That is a wonderful opportunity you have landed. Make sure you utilize the opportunity very well.
Mwengo: (Akitabasamu) I will. I am very happy.

Afisa: What criteria was used to select the students going for this scholarship?
Mwengo: Well, they picked two top students from every ward. A girl and a boy. They also ensured that the selected students were from poor backgrounds.
Afisa: What did you score in your K.C.S.E exams?
Mwengo: (Akitabasamu kwa fahari) I got a C plus of fifty eight points.
Afisa: Are your parents a live?
Mwengo: Yes, both of them are a live.
Afisa: Can I have their ID card copies?
Mwengo: Mama alipoteza ID yake. But I have brought her waiting card, since she has already applied for another one. I have also come with a copy of her police abstract that she was given when she went to report the loss. I hope those will help. As for my father, I have brought his copy of the ID. I hope those will be of some help.
Afisa: (Akikagua stakabadhi alizopewa ndani ya bahasha) Na hii copy ya kitambulisho cha mamako umetoa wapi? Si umesema mama alipoteza kitambulisho chake?
Mwengo: Mama alipoteza ID yake but before that time I had already made a copy of her ID.
Afisa: Leta hiyo waiting card na police abstract. Hiyo ndiyo *proof* kwamba anangoja kitambulisho kingine baada ya kuripoti kwa polisi kuwa kile alichokuwa nacho cha kwanza kilipotea.
Mwengo: (Akimkabidhi) Hizi hapa.
Afisa: Haya, sawa kabisa. Mwengo!
Mwengo: (Akiitika) Naam!
Afisa: Utaenda pale nje kwa photocopy utoe copy ya hizi mbili (akimpa) Kwa sababu tutakurudishia originals. Na wapi original birth certificates yako na za wazazi?
Mwengo: Yangu hii hapa. Wazazi wangu hata hawana *birth certificates*. Even me I got mine when I was registering for my K.C.P.E exams.
Afisa: How many are you in your family?
Mwengo: Well, we are seven of us.
Afisa: Can you name for me all the members of your family.
Mwengo: I am Mwengo Athman and Iam the first born. Then there is Hamisi Athman, Rajab Athman, Aisha Rukia Athman, Halima Athman, Mngumi Athman and finally there is Ramadhan Athman.
Afisa: Who among them has got the national Identity card?
Mwengo: None of them except me who is above eighteen. I am the only one with my parents who has an ID.
Afisa: (Akikagua fomu ya maombi ya pasipoti) Where is the recommender's ID copy? I can see the school rubber stamp. Did the Headmaster give you his ID copy?
Mwengo: No it is the Deputy Headteacher who signed and here is his ID copy.
Afisa: (Akipokea) Good. Give me your three passport size photos.
Mwengo: (Akimpa) Hizi hapa.

Afisa: (Anaanza kuzibandika kwenye fomu ya maombi ya pasipoti) Na wapi barua kutoka shuleni?
Mwengo: Ndio hiyo hapo. Na hili hapa jina langu (akionyesha jina lake katika orodha ya majina katika barua hiyo)
Afisa: Good, you are very lucky to get this opportunity. Make sure you utilize it maximumly.
Mwengo: Thank you sir, I will definitely work very hard.
Afisa: What are you going to study in India?
Mwengo: B.Com. Bachelor of Commerce. I want to study Bachelor of Commerce in India because Indians are very good businessmen.
Afisa: All the best young man. Now go get me copies of these documents as fast as you can. There is a photocopier outside the gate on your left.
Mwengo: (Akiondoka) Thanks sir. I will be back in a while.
(Baada ya dakika chache)
Hizi hapa nimeleta. I have infact made an extra copy for each.
Afisa: Its okay, you can keep the extra copy for your future use. You might still need them somewhere else. (Anazipanga karatasi zote huku akizikagua vizuri. Baadaye anampatia)
Haya, hizi hapa. You can now proceed to counter number three. From there you will be directed to the next stage. Congratulations once more for being considered for the academic scholarship.
Mwengo: (Akizipokea stakabadhi) Thanks a lot, I promise to work hard in my studies. (Anaondoka)

**Kiambatisho cha Pili**

Yafuatayo ni mazungumzo mafupi kuhusu tangazo lililotolewa na afisa wa idara ya uhamiaji kwa watu waliokuwa afisini. Ni tangazo lililonuiwa kupunguza watu pale afisini kwa kuwaondoa wale ambao hawakuwa na shughuli pale.

> Afisa: Aah, Samahani kidogo. *Excuse me.* Ikiwa uko hapa hii sehemu ya kukagua documents nisikize kidogo kuna tangazo. Kama umeleta mtu mzima, and by that I mean someone who is above eighteen years, awe mwanao, rafiki yako, jirani yako, whatever that person is to you na si wewe una apply for a passport please tunakuomba utoke nje.
> *I will repeat, please* ikiwa umeleta mtoto, na ana miaka zaidi ya kumi na nane, kwako anaweza kuwa mtoto lakini kwetu sisi huyo ni mtu mzima. Kama ana kitambulisho cha kitaifa tafadhali mwache kwa neema umsubiri pale nje. Ikiwa umeleta rafiki, jirani au hata mtoto bora ana ID mwache mwenyewe ajisimamie.
> Aaah, *in a moment* ikiwa tutakupata hapa ndani na hauna shughuli yoyote haitakuwa vizuri. *We want to discourage idling in this room and you might not like it if found doing nothing here. Thank you all.*

**Kiambatisho cha Tatu**

Yafuatayo ni mazungumzo yaliyohusisha wasichana wawili ambao familia yao ni ya asili ya Kiarabu na afisa wa Idara ya Uhamiaji Mombasa.

Afisa: Karibu. Ninahudumia mtu mmoja mmoja. Nani wa kwanza kati yenu?

Samira: No, we are sisters and we are together.

Afisa: Its okay, but then only one will sit because I only have one seat here.

Samira: Its okay, I will remain standing and my elder sister Shamsa here will sit.

Afisa: Haya karibu. Tutumie lugha gani, Kiingereza au Kiswahili?

Shamsa: Let's use English please. We are more comfortable with English.

Afisa: Right then. You are welcome.

Shamsa na Samira: (Kwa pamoja) Thank you. (Shamsa anaketi huku Samira akiendelea kusimama)

Afisa: Can I have your original documents plus the application forms you filled?

Shamsa: (Akimpa) Of course, here you can have them. They are all in this envelope.

Afisa: Thank you. (Anazitoa ndani ya bahasha na kuanza kuzikagua) Aaah, let me start with this one. Samira Shaneez. Samira, how old are you?

Samira: I am nineteen but will be turning twenty in May.

Afisa: Can I have your original Identity card?

Samira: Here, (akimpatia) here it is here.

Afisa: (Akikagua cheti cha kuzaliwa na kitambulisho kwa kuvilinganisha) Fauzia ndiye mamako?

Samira na Shamsa: Yaap, that's our mum.

Afisa: Do you have a copy of her ID?

Shamsa: It's among those documents we have given you. It was in that envelope.

Afisa: (Akiitafuta miongoni mwa Karatasi nyingine) Yaa, here I got it. Do your parents have passports?

Shamsa: Yes, both our parents have passports but we don't have. That's why we have come to apply because we are supposed to travel to Germany next month.

Afisa: This is good. I see you have brought copies of their passports. And this, this is a copy of your mother's birth certificate. Are your parents' Arabic?

Shamsa: Yes, we are Arabic.

Afisa: Do you two speak Arabic?

Shamsa na Samira: Yes.

Samira: But not very fluently.

Afisa: (Kimzaha) Can I apply for a few lessons in that?

Shamsa: Of course, why not?

Afisa: Where do you stay? I mean where is your home?

Samira: We stay in Guraya.

Shamsa: Guraya Majengo.

Samira: Yes, it's Guraya Majengo.

Afisa: How many are you in your family?
Shamsa: We are five including the two of us. That's our parents, our younger brother and the two of us.
Afisa: Samira, where were you studying in primary school?
Samira: Star of the Sea Academy.
Afisa: (Akiandika) Secondary?
Samira: Coast Girls.
Afisa: When did you sit your K.C.S.E exams?
Samira: Last year.
Afisa: Have you joined college?
Samira: Not yet. I will be joining a Germany University. That's why I need the passport.
Afisa: What work do your parents do?
Shamsa: Our father is a car dealer but our mother is just a housewife.
Afisa: What about your younger brother, his name and where is he?
Shamsa: He is Gudle and he is studying in Fadhili Academy. He is now in class six.
Afisa: (Akimuuliza Samira) Why don't you carry on your studies here in Kenya?
Samira: My aunt is in Germany and she had promised to take me upon finishing my high school and passing exams. She has already gotten a college for me.
Afisa: (Akipanga vizuri stakabadhi za Samira) Your photos, passport size photos. Where are they?
Samira: (Akimpa) Here, three of them.
Afisa: (Akipokea) Thanks. Nice photos. (Anazibandika kwenye fomu ya maombi ya pasipoti) I think yours are okay unless something comes up later on.
Samira: My father said the papers were in order and therefore I don't expect a problem to come up later on.
Afisa: (Akimpa Samira stakabadhi zake) From here you will go to counter number three or number four. Now let's see if your sister Shamsa is safe. Shamsa your original ID please!
Shamsa: (Akimpa afisa kitambulisho chake) Here. And of course if my sister is safe then Iam also safe.
Afisa: (Akikagua stakabadhi za Shamsa) Where is a copy of your birth certificate? I can't see it among these documents.
Shamsa: (Akionyesha kwa kidole) It's there, look there.
Afisa: Not this, this one is Samira's. Yours is not among these documents.
Shamsa: But this is my original birth certificate. You see this one here.
Afisa: The original birth certificate is here but what I am asking for is a copy of the certificate.
Shamsa: It was just among those.
Afisa: Samira!
Samira: yees.

Afisa: (Akimpa cheti cha kuzaliwa cha Shamsa) Here, run to the photocopy shop out there and make a copy of this certificate. Can you run like a student?
Samira: (Akipokea) Where is the photocopy?
Afisa: Outside the gate on your right. Just a few metres from the gate. Now off, I hope you have a few coins with you, it is not for free.
Samira: It's okay. I will be right back in a while. (Anaondoka)
Afisa: Shamsa, how old are you?
Shamsa: I am twenty three.
Afisa: What do you do?
Shamsa: Iam a student at the Nairobi College of Aviation Mombasa campus.
Afisa: I see it's like you want to join the aviation industry.
Shamsa: Yaap, I would like to be an air hostess.
Afisa: Where were you studying in secondary school?
Shamsa: Coast Girls, just like my sister.
Afisa: Was it a must that you study in the same school?
Shamsa: No, Samira liked the school so much when I was a student there. She vowed to study there after clearing her primary school and true to her word that's what she did.
Afisa: Your photos, where are they.
Shamsa: (Akimpatia) Here, they are here the three of them.
Samira: (Akimpatia afisa nakala aliyoleta) Here I brought two copies. And the place is far. Why don't you people have a photocopier here? It's very unfair to send people that far just for a photocopy.
Afisa: (Akipokea) Thank you Samira. As for the photocopy, we expect the applicant to come with all the required documents and therefore we don't anticipate sending you to the photocopy.
Samira: So many people are being sent there to make copies. I think someone should open a photocopy here. He can surely make a lot of money.
Afisa: Point noted Samira, but we don't encourage people doing business in this area, it might be a security risk you know. Now back to Shamsa, What is the colour of your eyes?
Shamsa: Why? I don't know.
Samira: (Akicheka) Why are you asking for the colur of her eyes?
Afisa: (Akionyesha) You mean you did not see this part of the application form? And if so then who filled this part for you?
Shamsa na Samira: (Wakiangalia kwa mshangao) Mmmmh! Aaaaah!
Afisa: Who told you that your eyes are red?
Shamsa: No my eyes are not red officer.
Afisa: Then what colour are they?
Shamsa: Mmmm, they are .... I dont know.
Samira: (Akimwangalia) Are mine white?

Afisa: (Akicheka) Your eyes are not white. No one has white eyes. When we talk of the colour of the eyes here, we mean the colour of the pupil of the eyes and not the whole eye. Now Samira look at Shamsa and tell me the colour of her eyes.
Samira: The pupil is blackish, brownish.
Afisa: (Akicheka) There is no such colour. Shamsa, what is the colour of Samira's eyes?
Shamsa: It's brown.
Afisa: Good. And that's also the colour of your eyes. Can both of you fill that part on your application forms then proceed to counter number three or four.
Shamsa na Samira: Thank you sir.
Afisa: You are welcome. Next person

**Kiambatisho cha Nne**

Mzungumzaji katika sehemu hii ni mama wa umri wa miaka sitini hivi. Aliletwa na mwanawe wa umri wa miaka arobaini hivi.

Afisa: Karibuni. Karibu. Niwasaidie namna gani?
Shaneez: Ahsante. Mimi naitwa Shaneez na huyu hapa Auntie yangu. Mamake na mamangu ndugu wa toka n'toke. Na sasa umwonavyo hivi ataka *passport*. Ataka *passport* aende kumtembelea mwanawe kule Uarabuni. Hivi utatusaidiaje?
Afisa: Sawa, karibu. Ashajaza *form* yake ya...
Shaneez: Kila kitu ashafanya. Hivi kwani wee hunijui? Mimi ni mtu wa hapa na siwezi kuleta kazi ambayo haijakamilika. Ni kama wewe hunijui sio.
Afisa: Kwani wewe unanijua?
Shaneez: Wewe mi hukuona lakini bado jina lako sijalijua. Utanipa jina lako na nambari ya simu...
Afisa: Unaona wewe hunijui na unatarajia mimi nikujue tu. *Anyway* hebu leta hizo *documents*.
Shaneez: *Form* hii hapa tushajaza kila kitu. Birth yake na kitambulisho hizi hapa na karatasi hizo zingine pia.
Afisa: (Akimlenga mama) Jina lako nani mama?
Fatuma: Mimi naitwa Fatuma.
Afisa: Nyumbani ni wapi?
Shaneez: (Akikatiza) Huyu kwao.....
Afisa: Shhhhh! Acha mama mwenyewe ajibu maswali haya. Nimwonavyo anaweza kujibu bila ya shida yoyote.
Shaneez: Sawa tu!
Afisa: Hivi Fatuma, nyumbani ni wapi?
Fatuma: Mimi nimezaliwa Kilifi lakini naishi Mombasa Tudor na mume wangu.
Shaneez: Mumewe ndiye anaishi naye hapa Mombasa.
Afisa: Umewahi kuwa na pasipoti hapo kabla au hii ndiyo ya kwanza?
Fatuma: Hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuhitaji pasipoti.

Afisa: Mbona unahitaji pasipoti?
Fatuma: Mwanangu wa kwanza aitwa Fatma aishiye kule Saudia amenialika huko.
Afisa: Nipe hizo stakabadhi zako.
Shaneez: Hizi hapa, zote zimo humo ndani ya bahasha hii.
Afisa: (Akizipokea) Ahsante. Kitambulisho chako *original* kiko wapi?
Shaneez: (Akimwambia Fatuma) Mpe hicho kitambulisho chako.
Fatuma: (Akimpa) Hiki hapa kitambulisho changu.
Afisa: (Akizikagua stakabadhi) Fatuma, hii *birth certificate* yako uliipata wapi?
Fatuma: Si ni kwa watu wa *births*? Kwani kuna nini?
Afisa: Tarehe yako ya kuzaliwa ni tofauti kama ilivyoandikwa katika *births* na katika kitambulisho. Je, ulizaliwa mwaka gani Fatuma?
Fatuma: Nafikiri ni mwaka wa arobaini na mbili. Waliniambia hivyo.
Afisa: Lakini huna uhakika.
Fatuma: Siku zetu hakukuwa na maandishi mengi kama ilivyo sasa.
Afisa: Tatizo ni kuwa katika *birth certificate* yako wameandika 1941 lakini katika kitambulisho wameandika 1942.
Shaneez: Ni kama kulitokea tatizo. Nikidhani unafaa kuwa mwaka wa arobaini na moja. Sababu ni kuwa huyu Fatuma hapa ni mkubwa wa mamangu. Naye mamangu kazaliwa mwaka wa arobaini na tatu. Hiki hapa kitambulisho cha mamangu.
Afisa: Basi kama ni hivyo watu wa vitambulisho walikosea kuandika arobaini na mbili. Yafaa tarehe hiyo irekebishwe.
Shaneez: Vipi sasa itarekebishwa na mama yuataka kusafiri? Yeye mwanzo amekaa na kitambulisho hiki hivi kwa miaka mingi tu. Atabadilishaje sasa?
Afisa: Unajua, tarehe ya kuzaliwa itakayoandikwa katika pasipoti ni lazima ilingane na ile ya *birth certificate* na ile ya kitambulisho. Hazifai kutofautiana.
Shaneez: Lakini sasa itakuwaje na hali mama anafaa kusafiri wiki ijayo, maskini mwonee mama huyu huruma.
Afisa: Sasa chukulia hivi Shaneez, ikiwa wewe ndiye mwenye kuchapisha pasipoti utaandika tarehe gani? Utaandika arobaini na moja au arobaini?
Shaneez: Hakuna njia yoyote unayoweza kutumia kutusaidia afisa?
Afisa: Umesema tarehe kamili ya kuzaliwa ni ile iliyoandikwa kwa *birth certificate* sio?
Shaneez: Naam, ile ya kitambulisho walikosea.
Afisa: Kwa hivyo inafaa mama arekebishe kitambulisho, wafahamu hivyo?
Shaneez: Hao watu wa vitambulisho hujikokota sana. Hivi kitambulisho kingine kupata ni hata ada ya mwaka.Sijui tufanyeje sasa.
Fatuma: Yaani siwezi kupata pasipoti hapa?
Afisa: Labda njia ya kuwasaidia ni moja tu.
Shaneez: Ipi hiyo? Tafadhali tusaidie.
Afisa: Itamlazimu Fatuma alete hati kiapo kutatua shida hiyo ya tarehe ya kuzaliwa.
Shaneez: Hiyo hati kiapo ndiyo nini?

Afisa: *Affidavit.* Huwa inaandikwa na lawyer. Itaeleza kuwa tarehe kamili ya mama kuzaliwa ni mwaka wa arobaini na moja na wala si mwaka wa arobaini na mbili kama ilivyoandikwa katika kitambulisho chake. Hiyo *affidavit* inafaa kuandikwa na *lawyer.*
Shaneez: Ni pesa ngapi hiyo *affidavit*?
Afisa: Haiwezi kuwa zaidi ya elfu moja. Lawyer yeyote tu anaweza kukuandikia *affidavit.* Ukileta hiyo *affidavit* tutakusaidia.
Fatuma: Na hiyo inachukua siku ngapi? Hiyo *fidavit.*
Afisa: Sasa hivi mkienda mtarudi nayo. Bora uende na kitambulisho na hiyo *birth certificate.*
Shaneez: Kuna kitu kingine kinachohitajika mbali na hiyo *affidavit*?
Afisa: Ngoja niangalie. (Akikagua stakabadhi) Huyu nani *aliyesign* hapa?
Shaneez: Ni Khamisi Kombo.
Afisa: Anafanya kazi gani?
Shaneez: Huyo ni chifu wetu anaishi pale Kibokoni.
Afisa: Basi inafaa aweke *rubber stamp ya chief* na awapatie *copy* yake ya kitambulisho. Nafikiri mko na *copy*?
Shaneez: *Copy* ametupatia tuko nayo lakini hiyo *rubber stamp* hakuweka. Tulimpata mjini na akasema ili kutia muhuri lazima awe afisini kwani huko ndiko kuna muhuri.
Afisa: Mtaenda huko afisini awawekee rubber stamp.Na pia ni muhimu kuleta copy ya kitambulisho cha dadake au ndugu yake.
Shaneez: Ninacho hiki hapa cha mamangu ambaye ni dadake wa toka nitoke.
Afisa: *Good.* Kwa hivyo nendeni mlete *affidavit* kisha *chief* aweke *rubber stamp* halafu mlete hizo *documents* kwa pamoja.
Fatuma: Halafu tukileta tutapata pasipoti hiyo siku?
Afisa: Ukileta tutakupatia *passport* baada ya wiki moja hivi. Sawa?
Shaneez: Hivyo atakuwa ashachelewa. Sikiza afisa. Sisi kesho tutakuletea hizo vitu zote. Halafu nataka utusaidie tupate hii pasipoti kabla ya hii wiki kuisha. Mama anafaa kusafiri Jumapili hii, na waona leo ni Jumatatu. Je, utatusaidia?
Afisa: Ikiwa mtaleta hizo *documents* basi nitawasaidia. Jaribuni sana mlete haraka kama kweli mnataka kusafiri haraka kama msemavyo.
Shaneez: Sawa, kesho asubuhi na mapema sisi tutakuwa hapa na kila kitu ulichosema. Halafu wewe utatusaidia kupata hiyo pasipoti haraka sio?
Afisa: Ni sawa.
Shaneez: *Your number please*, nisaidie namba yako ya simu. Nitakupigia *incase of anything.*
Afisa: Unataka namba ya ofisi au namba yangu?
Shaneez: Nipe namba yako, hiyo ya afisi halafu nani anisadie na hali hata simu yenyewe haichukuliwi?
Afisa: Bora ni saa za kazi huwezi kukosa mtu wa kukusaidia.Umewahi kupiga ukakosa kusaidika au unatuharibia tu jina?

Shaneez: Rafiki yangu Fatuma kaja hapa juzi, hata wiki mbili hazijaisha. Huyoo, mwenzako aliyekuwepo hapa kampatia namba, namba yenyewe kila akipiga yalia tu, hamna mtu anayemwitikia upande huo wa pili.Hiyo ndiyo namba unataka kunipatia? Mimi labda yako, hiyo ya afisi sitaki.

Afisa: Labda anayeshughulikia simu hakuwepo afisini.

Shaneez: Hiyo mimi sitaki.

Afisa: (Akiandika) Haya yangu hii hapa nakuandikia. (anampa karatasi)

Shaneez: (Akichukua) Nitaijaribu sasa hivi. Isipoingia narudi hapa.

Afisa: Hiyo ndiyo namba yangu ninayotumia kila wakati.

Shaneez: Haya kwaheri. Ahsante.

Afisa: Kwaheri

**Kiambatisho cha Tano**

Yafuatayo ni mazungumzo yaliyohusisha kijana wa miaka kumi na tisa hivi na babake wakihojiwa kwa zamu na afisa wa uhamiaji. Mahojiano haya yalikuwa ya kina kwa sababu ya utata uliozingira utaifa wa kijana huyu aliyekuwa ameleta maombi ya pasipoti ya Kenya.

Afisa: Karibu kijana. Wewe ulisema ulikuwa unakaa wapi?

Paul: Western.

Afisa: Wewe jibu vizuri maswali. Western upande gani?

Paul: Mumias.

Afisa: Ati na mama alikuwa anakaa wapi?

Paul: Tororo.

Afisa: Tororo Ug
anda?

Paul: Yes.

Afisa: Na wewe ulisema siku zako za utoto ulikuwa unakaa na mama?

Paul: Yes.

Afisa: Huko Tororo ndio ulikuwa unakaa na mama?

Paul: Yes.

Afisa: Tororo upande gani?

Paul: Tororo town.

Afisa: Halafu ukasomea wapi? Primary, AP one ulisomea wapi?

Paul: There in Tororo.

Afisa: Wewe hujui lugha ya Kiswahili?

Paul: I understand but I can not speak.

Afisa: Ulisoma hadi darasa gani?

Paul: Standard three.

Afisa: Ulisoma hadi class three why? Na ulikuwa unakaa na mama why?

Paul: There were some problems.

Afisa: Eeeh, which problems?

Paul: My mother got into a relationship with another man.
Afisa: Sasa wewe tangu uende na mama yako Uganda, uliwahi kuja Kenya?
Paul: No.
Afisa: Wewe haukuwa unakuja Kenya?
Paul: Mmmmh.
Afisa: Una hakika?
Paul: Yes.
Afisa: Mama alianza uhusiano na huyo Mgnda ukiwa na miaka mingapi?
Paul: When Iwas still young.
Afisa: Young miaka mingapi?
Paul: Not sure.
Afisa: Si ulisema ukiwa class three?
Paul: Yes.
Afisa: Nimekuita hapa ama umeletwa?
Paul: Nimeletwa na yule afisa.
Afisa: Sawa. Hapa utasema ukweli. Umekuja hapa kusema ukweli sio kudanganya. Nataka useme ukweli wako. Mama alikuwa anafanya kazi gani?
Paul: Business.
Afisa: What business?
Paul: I don't know.
Afisa: Mamako kwao ni wapi?
Paul: Nyeri.
Afisa: Alikwambia Nyeri ndio kwao?
Paul: Mmmh.
Afisa: Umewahi kwenda huko?
Paul: No.
Afisa: Hujui lugha ya Kikuyu hata neno moja? Hata kusalimia pekee huwezi?
Paul: I don't know.
Afisa: Huko Nyeri mama alikuwa anakaa na nani?
Paul: I don't know.
Afisa: Wewe kwa babako mlizaliwa wangapi.
Paul: I only know myself.
Afisa: Na kwa mama yako mko wangapi.
Paul: Iam alone.
Afisa: Wewe pekee yako? Umesema ulizaliwa pekee yako?Kenya ulirudi lini?
Paul: Am not sure.
Afisa: Sasa hiyo miaka yote, baba alikuwa anawatembelea huko Tororo.
Paul: Once in a while.
Afisa: Baba yako alikuwa akifanya kazi gani?
Paul: He was a footballer.

Afisa: Baba yako ni mzaliwa wa wapi? Kwao ni wapi?
Paul: Mumias.
Afisa: Kwa hivyo alikuwa akichezea timu ya Uganda?
Paul: Yes.
Afisa: Nani alikwambia hivyo?
Paul: My father's brother.
Afisa: Na wewe ulimjua baba yako lini?
Paul: When I was still young.
Afisa: Ulimjua vipi? As in nani alikujulisha kwa baba.
Paul: It was my mother.
Afisa: Wewe umewahi kwenda kwa akina baba huko Mumias?
Paul: Yes.
Afisa: Lini? Na ni Mumias sehemu gani.
Paul: It is in Shianda. I was there just before coming to Mombasa.
Afisa: Hebu niitie baba yako hapo nje. Kama umedanganya nitajua na hiyo itakuwa shida yako.

*Sehemu ifuatayo ya mazungumzo inahusisha mazungumzo baina ya mzee Shilesi na afisa wa idara ya uhamiaji. Mzee huyu ambaye ni mzazi wa Paul alihitajika katika afisi ili kuweka bayana maswala yaliyokuwa yakizua utata juu ya utaifa wa Paul. Baadhi ya sehemu katika mazungumzo haya zimefanyika kwa lugha asili ya Kiluhya.Hivi ndivyo mazungumzo hayo yalivyoendelea.*

Afisa: Habari yako mzee.
Shilesi: Mzuri.
Afisa: Wewe ndiye babake Paul?
Shilesi: Ndiyo ni mimi.
Afisa: Nisaidie kitambulisho chako mzee.
Shilesi: (Akimpa) Ndiyo hii hapa.
Afisa: Embolla kho.
(Hebu sema)
Shilesi: Malayi. Amalayi
(Good. Its good)
Afisa: Huyu mtoto wako alizaliwa lini?
Shilesi: Nafikiri ni 95.
Afisa: Yibe wakholanga kasi shina?
(Wewe ulikuwa unafanya kazi gani)
Shilesi: Mu hoteli (kwa hoteli)
Afisa: Kijana alisema kazi yako ni mpira
Shilesi: Nilipoumia mguu kwa mpira ndiyo nilianza kazi kwa hoteli.
Afisa: Mamawahuyu kijana wako anaitwa nani?
Shilesi: Milkah
Afisa: Mukhasi wo wokhuranga yalangwa wi?
(Mke wako wa kwanza alikuwa anaitwa nani)

Shilesi: Niye Milka uyoo. Yalangwa Milkah Nyambura.
(Ndiye huyo Milkah. Anaitwa Milkah Nyambura)
Afisa: Omwana uno yebulwa mwaka si?
Shilesi: Eighty-seven.
Afisa: Eighty-seven anohomba ninety-seven?
Shilesi: Eeeh, ni ninety-seven.
Afisa: Hujui mwaka ambao mtoto wako alizaliwa?
Shilesi: Ninety-seven.
Afisa: Mukhasi wo wadesia mwaka si?
(Mke wako ulimwoa mwaka gani?)
Shilesi: Enjichulilanga bulayi ta.
(Sikumbuki vizuri)
Afisa: Mukhasi nyina mwana uno mwadesiania lina? Hapa hakuna guesswork. Nataka ukweli.
Shilesi: Embaranga ni omwaka kwa ninety-five.
Afisa: Nyina mwana uno owabwe ni hena?
(Mama wa huyu mtoto kwao ni wapi?)
Shilesi: Nakuru.
Afisa: Nakuruali shina?
(Nakuu wapi?)
Shilesi: Londiani.
Afisa: Mwabukanila hena?
(Mlikutana wapi?)
Shilesi: Nakuru.
Afisa: Mwalekhana mwaka si?
(Mliachana mwaka gani?)
Shilesi: Mmmh, Eeeh,
Afisa: Hujui?
Shilesi: Yani shikhwatesiania bulayi tawe. Khwali shinga obulina.
(Yani hatukuoana vizuri. Tulikuwa kama marafiki.)
Afisa: Obulina bwenu bwawa mwaka si?
(Urafiki huo wenu uliisha mwaka gani?)
Shilesi: Lwakhanyola mwana uno.
(Wakati tulipopata mtoto huyu.)
Afisa: Wabukula mwana wo mwaka si?
(Ulichukua mtoto wako mwaka gani?)
Shilesi: Mwana yamenyanga na mama webe. Yakalukha mungo mwaka kuwele.
(Mtoto alikuwa akiishi na mama yake. Alirudi nyumbani mwaka uliopita)
Afisa: Mungo ni hena?
Shilesi: Mumias Shianda.
Afisa: Mubere banga owenywe.

(Mko wangapi kwenu?)

Shilesi: Basiani bataru nende bakhana babili.

(Wavulana watatu na wasichana wawili)

Afisa: Wote wako hai

Shilesi: Ndiyo.Wako Mumias.

Afisa: Sawa mzee. Unaweza kwuondoka

Shilesi: Orio muno. Kwaheri.

(Ahsante sana. Kwaheri.)

**Kiambatisho cha Sita**

Munyao: Wee Kasee wacha hizo. Hii kitu si *pend.*

Mueke: Sio mimi nasema, ni *system.*

Munyao: Kwani mbona mnasumbua Wakenya hivi? *You should be patriotic.*

Mueke: Wewe sin i Mkenya na tena *patriot,* saidia wao. Weka hapa *sign* ndio niamini.

Munyao: *You are subjecting innocent Kenyans to extreme scrutiny. Why?*

Violet: Patia Munyao hiyo *file* asaidie. Ni kama yeye alikuja hapa kusaidia.

Mueke: *He is just being naughty.*

Munyao: Sawa Madam Vio, I was just testing my brother here.

**Kiambatisho cha Saba**

Wamalwa: *Excuse me boss*, ile *case* ya Hajj tufanyeje?

Scolla: *Of course it has to go through the office. I hope* ame-*avail all the required documents.*

Wamalwa: Ndiyo *madam*, *but* hana barua ya *chief.*

Scolla: *You know very well requirements* za *Hajj applications*. Lazima applicant alete barua ya chief, barua ya *Council of Imams* au *Supkem*, *next of kin*, *ID copies and original ID & BC plus copies.*

Wamalwa: Sawa madam, *only chief's letter is missing.*

Scolla: Ambia *applicant* aende kwa *chief* aandikiwe hiyo barua halafu arudi.

Wamalwa: *Thanks madam.*

**Kiambatisho cha Nane**

Afisa A: Excuse me madam, boss to consult something.

Afisa B: Kwani wewe huoni niko busy, unapenda kunisumbua sana.

Afisa A: Sorry, ni hivi, hii bc haina authority number na ni late registration.

Afisa B: Kwanza hata bc yenyewe haina seal.

Afisa A: But my main aim ni ku establish ethnicity.

Afisa B: You start by looking at parentage. Kwani hujui hiyo wewe? Wazazi wake wanatoka wapi?

Afisa A: I have no idea madam.

Afisa B: Na sasa unataka mimi nitoe wapi hiyo idea? Wewe mambo ya kuniletea hapa vitu havieleweki sitaki. Tuma huyo mtu vetting afanyiwe thorough interview to establish his ethnicity. Wacha niendelee na kazi yangu.

Afisa A: Kwa hivyo recommendation yako ni further interview?

Afisa B: Of course, mtu yeyote ambaye roots zake ziko in doubt lazima aende for further scrutiny.

Afisa A: Thanks madam.

**Kiambatisho cha Tisa**

Afisa C: Hallo, naulizaje unangalilie hii kama R number yake ni same na ya babake.

Afisa D: Wapi passport number yake.

Afisa C: Hana ndio sababu nataka u track kwa system. Passport ilipotea.

Afisa D: Nani anataka passport?

Afisa C: Ni mtoto mdogo ndio sababu twatumia file ya babake.

Afisa D; Wapi valid passport ya baba? Lazima tuione.

Afisa C: Wacha basi nimwambie ailete.

**Kiambatisho cha Kumi**

Afisa E: Wee boss, uko wapi leo?

Afisa F: Niko counter five.

Afisa E: Kwani umetoka verification?

Afisa F: Ni vile nimeambiwa nishikie Savini coz ameenda vetting.

Afisa E: Sawa, please stapler.

Afisa F: Mary, ask Mary.

Afisa: E: Okay.